# INTERFAITH DIALOGUE IN TANZANIA




# WAJIBU WA MASHIRIKA YA DINI KATIKA KUHAKIKISHA UWEPO WA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI

Konrad Adenauer Stiftung

# INTERFAITH DIALOGUE IN TANZANIA

# WAJIBU WA MASHIRIKA YA DINI KATIKA KUHAKIKISHA UWEPO WA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI

**IMETOLEWA NA:**

**Inter Religious Council for Peace Tanzania**
**&**
**Konrad Adenauer Stiftung**

**Novemba, 2010**

ISBN: 978-9987-9276-6-1

© KAS. Haki zote zimeifadhiwa. Si ruhusa kutumia sehemu ya kitabu hiki kwa njia yoyote ile (ikiwa ni pamoja na kudurufu au kukiweka kwa njia za kielektronia, iwe ni kwa kukusudia au kwa kutokukusudia) bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye hakimiliki.

**Konrad-Adenauer-Stiftung (KAS)** wakishilikiana na **Inter Religious Council for Peace Tanzania (IRCPT)** waliratibu mjadala huu.

Mjadala huu umefadhiliwa na **Serikali ya Ujerumani** kupitia **Ubalozi wa Ujerumani nchini Tanzania.**

Konrad Adenauer Stiftung

S. L. P. 6992
Barabara ya Isimani, Upanga
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2153174
kas.tanzania@gmail.com

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| **Orodha ya Vifupisho** | ............................................ | v |
| **Wimbo wa Taifa** | ............................................ | vi |
| **Nukuu Kutoka Vitabu Vitakatifu Juu ya Uchaguzi Huru na wa Haki** | ......... | vii |
| **Shukurani** | ............................................ | viii |
| **Utangulizi** | ............................................ | ix |
| **SEHEMU A:** | **Ujumbe Kutoka Ofisi za IRCPT, KAS na FRG:** ............... | 1 |
| | Hotuba ya Katibu Mkuu, IRCPT ....................................... | 1 |
| | Hotuba ya Kiongozi wa KAS .............................................. | 3 |
| | Hotuba ya Naibu Balozi wa Ujerumani Nchini Tanzania ...... | 3 |
| **SEHEMU B:** | **Uwasilishaji wa Mada Juu ya Wajibu wa Masharika ya Dini Katika Kuhakikisha Uwepo wa Uchaguzi Huru na Wa Haki** ............................................ | 5 |
| | **Mada ya Kwanza:** Wajibu wa Masharika ya Dini katika kuhakikisha uwepo wa uchaguzi huru na wa haki ................. | 5 |
| **SEHEMU C:** | **Uwasilishaji wa Mada Juu ya Wajibu wa Masharika ya Dini Katika Kuhakikisha Uwepo wa Uchaguzi Huru na wa Haki** ............................................ | 25 |
| | **Mada ya Pili:** Nafasi ya Mashirika ya Dini Katika Uchaguzi Huru na wa Haki ............................................ | 25 |

**Maoni/Mapendekezo ya Wawakilishi wa Viongozi wa Mashirika ya Kidini Nchini Tanzania** ............................................ 45

- *Changamoto kwa Mashirika ya Dini* .................................... 45
- *Ushauri Kwa Serikali* .................................... 45
- *Michango Zaidi ya Wawakilishi:* .................................... 46
- *Katiba Iangalie Haki za Wazee na Watoto* .................................... 46
- *Suala la Watoto wa Mitaani* .................................... 46
- *Kuhusu Katiba* .................................... 46

**KUFUNGA:** **Mtazamo wa KAS Katika Mikutano ya Usoni ya IRCPT** .......... 48
**Je IRCPT ni Nini?** .......... 48
**Shukurani:** .......... 51

**VIAMBATISHI** .......... 52

**Kiambatishi 1: MADA ZILIZOWASILISHWA**

**1. Mada ya Bwana Bernard Okok-Obuoga** .......... 52
- *Imani za dini na mashirika ya dini katika jamii* .......... 54
- *Uzoefu wa Kenya* .......... 58
- *Mchango wa mashirika ya dini katika mchakato wa uchaguzi* .......... 61
- *Wito kuchukua hatua* .......... 63

**Kiambatishi 2: MADA ZILIZOWASILISHWA**

**1. Mada ya Ndugu Ebenezer Stafford Mshana** .......... 65
- *Chaguzi Huru na za Haki* .......... 66
- *Jukumu la Asasi za Kidini/Kiimani katika kuhamasisha Chaguzi Huru na za Haki* .......... 70
- *Utoaji wa elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura* .......... 71
- *Hitimisho* .......... 74

**MAREJEO** .......... 75

**ORODHA YA WASHIRIKI** .......... 76

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **ACRL-RfP** | - | African Council of Religious Leaders-Religions for Peace |
| **ACRL** | - | African Council of Religious Leaders |
| **BAKWATA** | - | Baraza Kuu la Wailsamu Tanzania |
| **CCT** | - | Christian Council of Tanzania |
| **CETA** | - | Civics Education Teachers' Association |
| **CPT** | - | Christian Professional of Tanzania |
| **FOBs** | - | Faith Based Organisations |
| **FRG** | - | Federal Republic of Germany |
| **IRCPT** | - | Inter Religious Councils for Peace Tanzania |
| **KAS** | - | Konrad Adenauer Stiftung |
| **NEC** | - | National Electoral Commission |
| **NIRCs** | - | African Inter-Religious Councils |
| **PCT** | - | Pentecostal Council of Tanzania |
| **SADC** | - | Southern Africa Development Community |
| **SIRCBs** | - | Sub-Regional Inter-Religious Coordinating Boards |
| **TAMPRO** | - | Tanzania Muslim Professionals |
| **TEC** | - | Tanzania Episcopal Conference |
| **TPDF** | - | Tanzania Peoples' Defence Force |
| **TADIP** | - | Tanzania Development Initiative Program |
| **UNO** | - | United Nations Organization |
| **UNDP** | - | United Nations Development Programme |
| **URT** | - | United Republic of Tanzania |

## WIMBO WA TAIFA

Mungu Ibariki Afrika
Wabariki Viongozi wake
Hekima Umoja na Amani
Hizi ni Ngao zetu
Afrika na watu wake

Ibariki Afrika Ibariki Afrika
Tubariki Watoto wa Afrika

Mungu Ibariki Tanzania
Dumisha Uhuru na Umoja
wake kwa waume na watoto
Mungu Ibariki
Tanzania na watu wake

Ibariki Tanzania Ibariki Tanzania
Tubariki watoto wa Tanzania

## NUKUU KUTOKA VITABU VITAKATIFU JUU YA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI

| | |
|---|---|
| <u>Judaism:</u> | *"Unachokichukia wewe; usimtendee mtu mwingine. Hii ni sheria. Mengine ni tahariri tu." Talmud, Shabbat 3 la.* |
| <u>Waislam:</u> | *"Hakuna kati yenu (kwa kweli) anaamini mpaka anapotaka kaka yake afikiwe na mazuri aliyoyapata yeye." Number 13 of Imam "Al-Nawawi's Forty Hadiths"* |
| <u>Imani ya Baha'i</u> | *"usimuombea mtu usichotaka mwenyewe kuombewa. Usimseme mtu kitu ambacho mwenyewe hungependa kusemwa."*<br><br>*"Mbarikiwa ni yule anayetaka kaka yake afanikiwe badala yake." Baha'u'llah* |
| <u>Wakristo:</u> | *"kwa hiyo katika yote, watendee wengine yote ambayo ungependa kutendewa mwenyewe kwani hili ni jumuisho la Sheria na Mitume" Matthew 7:12 (NIV)* |

## SHUKURANI

IRCPT na KAS wanatanguliza shukrani za dhati kwa madhehebu yote ya dini ambayo yaliweza kuwakilishwa katika majadiliano hayo na hivyo kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Shukrani pia ziwaendee washiriki wote kwa usikivu na michango yao wakati wa mjadala, iwe ya moja kwa moja au kwenye vikundi. Kitabu hiki kinatokana na michango ya mawazo yao.

Mwisho kabisa shukrani ziende kwa waratibu wa mjadala, na wale wote ambao michango yao haiwezi kuonyeshwa moja kwa moja.

## UTANGULIZI

Kutoka tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi Oktoba 2010, wawakilishi wa Viongozi wa Mashirika ya Dini yanayoshughulikia Amani nchini Tanzania (IRCPT) walikutana katika Hoteli ya Land Mark, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam kuzungumzia namna gani Uchaguzi Mkuu nchini utakuwa huru na wa haki.

Katika kuhakikisha kuwa lengo la wawakilishi hao la kutaka uchaguzi huru na wa haki linafikiwa, Wafadhili wa mkutano huo, taasisi ya Ujerumani ya Konrad Adenauer Stiftung, KAS, iliwaleta wawezeshaji wawili kutoka nchini Kenya na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao waliwasilisha mada za kusisimua zilizokuwa na uhusiano na malengo ya kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu unakuwa huru na wa haki.

Ndugu Bernard Okok-Obuoga kutoka Baraza la Viongozi wa Dini wa Afrika-Dini kwa Alili ya Amani, nchini Kenya aliwasilisha mada katika mkutano huo.

Mada hiyo ilikuwa na kichwa kifuatacho kuhusu: Nafasi ya Mashirika ya Dini katika kuhamasisha uchaguzi huru na wa haki (uzoefu wa Kenya).

Mbali na kutoa ushauri kwa IRCPT, juu ya namna shirika hilo lingeweza kufikia lengo lake la kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu unakuwa huru na wa haki, Ndugu Okok aliwaambia wajumbe katika mkutano huo chimbuko la mapigano yaliyotokea nchini Kenya mara baada ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mkwaka 2008, ushiriki wa Shirika la Dini nchini Kenya katika mgogoro ule na namna mapigano hayo yangeweza kuepukika.

Kwa kifupi, Ndugu Okok alieleza kwa kirefu nafasi ya IRCPT, kama taasisi ya mashirika ya dini, katika kushughulikia migogoro ya kisiasa nchini Tanzania na namna shirika hilo la dini lingeweza hatimaye kuhakikisha kuwa chaguzi nchini Tanzania zinakuwa huru na za haki.

Kwa upande mwingine, mwezeshaji kutoka nchini Tanzania, Ndugu Ebenezer Mshana, ambaye ni Mhadhiri wa Sheria katika Shule ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alitumia mada yake ambayo ilikuwa na kichwa sawa na ile iliyotolewa na Ndugu Okok, kwa kuangalia suala la chaguzi huru na haki kutoka mtazamo wa kimwanazuoni.

Ndugu Mshana alitoa ushauri kutumia vigezo ambavyo alisema utekelezaji kikamilifu wa vigezo hivyo ndio ulikuwa unatoa jibu kama nchi husika imefanikiwa kuwa na uchaguzi huru na wa haki au la.

Hata hivyo, hali ya hewa ya mkutano huo nusura iingie dosari katika siku yake ya kwanza tu, pale ulipojitokezo upepo wa kutoaminiana na wasiwasi miongoni mwa wajumbe.

Hata hivyo kujitokeza kwa upepo huo halikuwa jambo la ajabu, kwani hali hiyo mara kwa mara hujitokeza katika mikutano ya wafuasi wa dini mbalimbali kila wanapokutana kujadili namna ya kutatua matatizo ya kijamii kwa kutumia majukwaa yao ya pamoja ya kidini.

Lakini kwa bahati nzuri, kila mkutano huo ulipokuwa ukiendelea, ndivyo wawakilishi wa viongozi wa dini katika chama hicho cha IRCPT, walipokuwa wakigundua juu ya umuhimu wa wao kuzingatia zaidi kitu kilichokuwa kimewapeleka katika mkutano huo, yaani kushughulikia mkakati mpango wa namna ya kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu nchini Tanzania ulikuwa huru na wa haki.

Mabadiliko ya mtazamo huo, kwa kiasi kikubwa, yalichochewa na zile mada mbili ambazo zilikuwa zimetolewa katika mkutano huo na wale wawezeshaji wawili, ndugu Okok kutoka Kenya na Ndugu Mshana kutokana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hali ya hewa mpya ya udugu miongoni mwa wajumbe katika mkutano huo, hatimaye ilisaidia kuwaongoza wajumbe hao kuwa na mazungumzo ya tija, hali ambayo baadaye iliwasaidia katika kujikusanyia maoni na mawazo mbalimbali kwa nia ya kuhakikisha kuwa chaguzi nchini zinakuwa huru na za haki.

Ijapokuwa wawakilishi hao wa viongozi wa dini wa IRCPT hawakuweza kutoa mchango wao katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kutokana na muda mfupi wa matayarisho kabla ya uchaguzi huo.

Hata hivyo walifanikiwa, kwa kiasi kikubwa, katika kuunda jukwaa ambalo baadaye litasaidia sana katika kutatua migogoro mbalimbali nchini na hivyo kufanya chaguzi kuwa huru na za haki.

Ni kutokana na hali hiyo, wasomaji wetu wataona tofauti katika chapisho hili, kwa namna fulani na lile lililopita, kutokana na uundwaji wa maandishi yake.

Moja ya tofauti hizo ni kwamba wachangiaji wote katika mkutano ule ukiondoa Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Ndugu Hans Koeppel na Katibu Mkuu wa IRCPT, Ndugu Ayoob Omari, tumetumia Ndugu badala ya vyeo vyao.

Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kuendeleza hali ya hewa ya uelewano na udugu iliyokuwa imejitokeza katika mkutano ule.

Tunaamini kuwa mwendelezo wa hali ile, utasaidia pia katika kutatua matatizo mbali mbali ambayo yanaisumbua nchi yetu ya Tanzania.

Hata hivyo, majina ya wachangiaji katika mkutano ule tumeyaweka katika kurasa za mwisho za chapisho hili kwa nia, pamoja na mambo mengine, ya kuonesha watu wote ambao walihudhuria mkutano ule kwa nafasi mbalimbali.

Uamuzi wetu wa kutotumia vyeo vya wachangiaji katika mkutano ule ni kwamba tunafikiri kuwa wale waliyoyasema wachangiaji hao yana maana kubwa zaidi kwa jamii kuliko vyeo vyao. Kwa kifupi tunataka watu watofautishwe kwa mawazo na sio kwa vyeo walivyonavyo.


Ni matumaini yetu kuwa utafaidika na kuburudika na michango mbali mbali katika kitabu hiki.

## SEHEMU A:

## UJUMBE KUTOKA OFISI ZA IRCPT, KAS NA FRG:

### 1. HOTUBA YA KATIBU MKUU, IRCPT, NDUGU AYOOB OMARI

Msisitizo mkubwa juu ya haja ya mashirika ya dini kuhakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki nchini uliwekwa kwenye ufunguzi wa mkutano wa siku tatu wa viongozi wa mashirika ya dini (IRCPT) uliofunguliwa kwenye ukumbi wa mkutano wa hoteli ya Landmark, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam tarehe 11, Oktoba, 2010.




Mkutano huo ulioandaliwa na IRCPT na kugharamiwa na taasisi ya kimataifa ya Ujerumani yenye ofisi yake mjini Dar es Salaam, Konrad Adenauer Stiftung, (KAS), ulikuwa ukifanyika siku 20 tu kabla ya kufanyika nchini kwa uchaguzi mkuu, tarehe 31, Oktoba, 2010.

Kabla ya kumkaribisha Naibu Balozi wa Ujerumani hapa nchini, Ndugu Hans Koeppel, kufungua rasmi mkutano huo, Katibu Mkuu wa IRCPT, Ndugu Ayoob Omari, alisisitiza juu ya kutumia mazungumzo katika utatuzi wa migogoro ya aina yoyote ile inayoikabili jamii.

"Njia pekee ya kutatua migogoro na hivyo kujenga amani nchini ni kupitia mazungumzo. Amani na haki ni vitu muhimu kwa jamii na vinakwenda pamoja. Bila amani hakuna haki. Kadhalika, bila haki hakuna amani," alisisitiza.

Kwa mfano, alisema kushindwa kwa viongozi wa dini kuchukua hatua za haraka kushughulikia migogoro na mifarakano inayojitokeza ndani ya jamii kunaweza kuleta hatari kubwa kwa taifa.

Ndugu Omar alisema tatizo hilo liliwakumba viongozi wa Kikristo katika mji wa Jos, kaskazini mwa Nigeria pale baadhi ya waumini wao walipowaua wafanyabiashara wa kiislamu ambao walikuwa wakifanya biashara mjini Jos.

Alieleza kuwa wakazi wa mji huo walikuwa wakristo, lakini wafanyabiashara walikuwa waislamu ambao kwa kawaida walikuwa wakiishi nje ya mji huo.

Akizungumzia tukio hilo la kutisha na kusikitisha, Ndugu Omari alisema mara baada ya mauaji hayo, viongozi wa Kikristo walikaa kimya badala ya kulaani vikali vitendo hivyo.

Ukimya huo uliwafanya waislamu kuamini kuwa wauaji wale walikuwa wakiungwa mkono na viongozi wao jambo ambalo liliwafanya kulipiza kisasi.

Ndugu Omari alisema kuwa matokeo ya kisasi kile ndio yale dunia inayoshuhudia hivi sasa yakiendelea kaskazini mwa Nigeria, mapigano ya mara kwa mara kati ya Waislamu na Wakristo baadaa ya viongozi wa Wakristo kushindwa kukemea tokio lile walilolifanya waumini wao.

Waislamu pia walikuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Kitu kikubwa ambacho viongozi wa Wakristo walitakiwa kufanya baada ya kutokea kwa mauaji yale ni kukemea vikali tukio hilo.


Akizungumzia juu ya uchaguzi mkuu nchini Tanzania, Ndugu Omari alisema kuna haja kubwa kwa watu kuelewa kuwa ushindi katika uchaguzi unategemea sana matayarisho ya kina katika nyanja tofauti.

Alizitaja nyanja hizo kama matayarisho kutoka katika ngazi ya chama cha siasa, uteuzi wa wagombea ndani ya chama, uandikishaji wa wapiga kura na mwisho kupiga kura, kuhesabu na hatimaye kuwatangaza washindi na walioshindwa.

Alionya kuwa makosa yoyote yanayofanywa katika nyanja yoyote ile aliyoitaja yalikuwa na athari ya kutoa picha mbaya hasa matokeo ya uchaguzi yatakapotangazwa.

Alisema mipango mibovu ya matayarisho inakuwa ni hatari, wakati fulani wahusika kubeba picha kuwa wameshinda wakati ukweli ulikuwa tofauti.

## 2. HOTUBA YA KIONGOZI WA KAS, RICHARD SHABA




Umuhimu wa mazungumzo katika utatuzi wa migogoro ulisisitizwa pia na kiongozi wa timu ya KAS, Ndugu Richard Shaba.

Alisema ijapokuwa katika mkutano wa viongozi wa dini uliofanyika mwaka jana ulikuwa na mivutano mingi kati na baina ya viongozi hao, lakini mwisho kulikuwa na maelewano na mkutano huo ukamalizika salama.

Ndugu Shaba alisema yote hayo yalitokana na kufanikishwa kwa mazungumzo.


Alisema mazungumzo ndio yaliyosaidia katika kuwafanya wajumbe hatimaye kuelewana.

Kutokana na tukio lile, Ndugu Shaba alisema kuwa yalikuwa matumaini yake kuwa mkutano ambao ulikuwa karibu kuanza pia ungeweza kufanikiwa kama ule uliopita, kupitia majadiliano.

## 3. HOTUBA YA UFUNGUZI YA NAIBU BALOZI WA UJERUMANI NCHINI TANZANIA NDUGU HANS KOEPPEL

Naye mgeni rasmi aliyeufungua rasmi mkutano huo wa viongozi wa dini, Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Ndugu Hans Koeppel, akaweka msisitizo mwingine katika dhana ya mazungumzo kama njia pekee ya utatuzi wa migogoro na mifarakano katika jamii.

"Mimi binafsi nayawekea uzito na thamani kubwa mazungumzo kama njia muafaka ya kutatua migogoro," alisema mwana diplomasia huyo.




Akiungana na Ndugu Omari juu ya matatizo ya kidini kaskazini mwa Nigeria, Ndugu Koeppel alisema alikuwa kikazi, mjini Kano, nchini Nigeria wakati mapigano na mauaji yakitokea katika nchi hiyo ya Afrika ya magharibi.

Balozi Koeppel aliishukuru taasisi ya KAS kwa kugharamia mkutano huo wa viongozi wa dini.

Naye akaahidi kuwa ubalozi wa Ujerumani utatoa msaada wa aina hiyo hapo mwakani.

Alisema yakiwa yamebaki majuma machache tu kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu, tayari kulikuwa kumeshuhudiwa mivutano midogo midogo ya kisiasa hapa na pale kati na baina ya wagombea viti mbalimbali hapa nchini.

Lakini alisema jambo la kufurahisha ni kwamba kwa mara ya kwanza katika historia, wananchi wa visiwa vya Zanzibar watakuwa wanapiga kura ya kuchagua serikali ya mseto.

“Kwa mara ya kwanza, hatutashuhudia mfumo wa mshindi katika uchaguzi kuchukua kila kitu na kumuacha mwenzake ambaye pengine wametofautiana kidogo sana, akiondoka mikono mitupu,” alisema Ndugu Koeppel.

Alisema Ubalozi wa Ujerumani hivi sasa ulikuwa unagharamia tume ya watu sita ya Zanzibar ambayo ilikuwa ikitembelea Uingereza na Ujerumani kwa nia ya kujifunza namna nchi hizo mbili zinavyoendesha serikali za mseto/umoja wa kitaifa.

**SEHEMU B:**


# UWASILISHAJI WA MADA JUU YA WAJIBU WA MASHARIKA YA DINI KATIKA KUHAKIKISHA UWEPO WA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI

## 1. MADA YA KWANZA
**Wajibu wa Masharika ya Dini katika kuhakikisha uwepo wa uchaguzi huru na wa haki**

### NDUGU BERNARD OKOK-OBUOGA: MUISHI KWA KUSAIDIANA

Mada ya kwanza kwenye mkutano huo iliwasilishwa na Ndugu Bernard Okok-Obuoga kutoka Baraza la Viongozi wa Mashirika ya Dini Barani Afrika (ACRL), nchini Kenya.

Kuhusu nafasi ya Mashirika ya Dini katika kusimamia kuwepo nchini kwa Uchaguzi huru na wa Haki na uzoefu wa Kenya katika Uchaguzi Mkuu uliopita, Ndugu Okok-Obuoga alisema shirika moja pekee la kidini haliwezi kufanya mabadiliko nchini, kama vile kuhakikisha uwepo wa uchaguzi huru na wa haki.



Alisema ili mashirika ya dini yafanikiwe katika kuleta maendeleo ya kitaifa nchini, ilikuwa lazima mashirika hayo kushirikiana kwa karibu sana.

Akizungumzia juu ya matatizo, alisema mashirika ya dini yalikuwa yanapaswa kufahamu kuwa tatizo linapoingia nchini, huwa haliji kwa sura ya kidini.

Hata hivyo, alisema athari na hata tatizo mbali na kuwa baya, kwa kawaida athari na tatizo halijali mtu alikuwa mfuasi wa imani gani linapoanza kuleta kero yake.

Aliwachekesha washiriki kwenye mkutano huo wakati aliposema waumini wa dini mbalimbali wakiwekwa katika chumba kimoja na simba mwenye njaa, ni dhahiri kuwa mnyama huyo atamshambulia mtu bila kujali alikuwa anatoka imani gani.

Njia ya pekee ya kujiokoa kwa waumini hao dhidi ya simba aliyejitokeza miongoni mwao ni kwa waumini hao kushirikiana katika kupambana na kumuua simba huyo.

Kadhalika, alisema hiyo ndio njia ya pekee mashirika ya dini yanapaswa kutumia katika kupambana na matatizo mbalimbali yanayowakabili na hivyo kujiletea maendeleo na amani nchini mwao.

Ndugu Okok pia alisisitiza juu ya haja ya mashirika hayo ya dini kuongozwa, katika jitihada zao za kutatua migogoro na hivyo kujiletea maendeleo, na dhana ya ukweli.

Alilinganisha matumizi ya lugha ya uongo na kijana ambaye katika nia yake ya kumpata mwanamke, anajikweza kwa kusema uongo, kwa mfano, kuwa yeye hakuwa na matatizo ya kifedha kwamba alikuwa tajiri.

Tatizo la kusema uongo, alisema Ndugu Okok-Obuoga ni kwamba haitapita muda mrefu yule mwanamke atajua ukweli kuhusu yule kijana.

"Siku zote ni vizuri kuanzia kwenye msingi imara, msingi wenye ukweli. Ukweli siku zote utakupa uhuru. Tunapaswa kuacha kusema uongo," alisisitiza.

Akizungumzia juu ya yaliyotokea nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2008, ambapo zaidi ya watu 1,000 waliuawa, alisema kuwa maafa yale yangeepukwa kama viongozi wa dini nchini humo wangekuwa walisimamia masuala fulani kikamilifu.

Aliwalaumu viongozi wa dini nchini Kenya kwa kuendeleza ukabila na ubinafsi badala ya kushirikiana katika kutatua matatizo ya nchi.

Aliwataka viongozi wa dini nchini Tanzania kujikinga na yale waliofanya wenzao nchini Kenya kwa kujijengea mshikamano utakaowasaidia katika kutatua matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayoikabili nchi yao.

"Kama kiongozi wa dini, unapaswa kutojihusisha na vitu vidogo vidogo. Jitahidi kuwa muadilifu, hata kama mwanasiasa mwenye matatizo anatoka katika dini yako, usimuonee haya. Muwajibishe. Na huo ndio uongozi wa kiadilifu.

Pili hakikisha kuwa unamshughulikia kwa kutumia mjadiliano," alisisistiza.

Lakini ili wawe na mafanikio, alisema mashirika ya dini yalipaswa kutumia dhana za ushirikiano, ukweli na kukubali uwepo wa tofauti zao, pamoja na zile za imani zao.

Alisema katika dhana ya utofauti, viongozi wa dini wanapaswa kukubali kuwa dini zao ziko tofauti. Lakini kikubwa, ni kutambua hilo na kuliheshimu.

"Hampaswi kuzika tofauti zenu, la hasha; bali kutambua uwepo wa tofauti hizo," alisisitiza.

Alisema kwa kutambua na kukubali tofauti ya dini, kati ya dini yako na ile ya mwenzako na kuheshimu, uaminifu kati ya pande hizo mbili hujengwa na hatimaye kuzaa urafiki.

Chini ya mwavuli wa urafiki, alisema, sasa huwa rahisi sana kutatua matatizo yanayowakabili.

Hivyo hivyo, alisema, ilikuwa katika dhana ya ukweli. Watu siku zote humpenda msema kweli, watu humwamini kwa kuwa wakati wote mtu huyo huwa hana ajenda yoyote ile ya siri!

Kutokana na hilo, Ndugu Okok alisema ilikuwa rahisi kwa watu au viongozi wa mashirika ya dini yanayofuata dhana hizo mbili kuaminiwa na mashirika mengine ya dini.

Lakini akatoa tahadhari kuwa vitu hivyo viwili haviwezi kukamilika bila kuwa na dhana ya majadiliano (engagement) ya pamoja na ya mara kwa mara.

Dhana nyingine ambayo ilikuwa muhimu kwa matumizi, alisema, ilikuwa ile ambayo ilikuwa inaelezwa mara nyingi katika vitabu vitakatifu.

Kwa kifupi dhana hiyo inasema 'usimtendee mwenzio kitu ambacho wewe hungependa kutendewa'.

Dhana hiyo ilikuwa inafuatiwa kwa karibu na ile ya kuishi sio tu na mwenzako, bali kwa ajili ya mwenzako.

Dhana hii inasimamia suala zima la utayari wa kumsaidia au kwasaidia wenzako, dhana ya kusimama upande wa wanyonge.

Kwa wakristu, dhana hii huhusishwa na mafunzo yaliyomo katika Biblia wakati Yesu alipoletewa mwanamke aliyedaiwa kuwa alikutwa akizini.

Yesu akawauliza wanaume waliokuwa wamemleta kwake mwanamke yule ni adhabu gani mtu kama yule hupewa.

Nao wakamjibu kuwa mwanamke huyo alipaswa kupigwa mawe mpaka kufa.

Naye akawaambia yoyote yule ambaye hajawahi kufanya kitendo kile, basi achukue jiwe na kuanza kumpiga mwanamke huyo.

Baada ya kusema hivyo, alianza kuchora chini.

Lakini alipoinua kichwa baadaye, yule mwanamke alikuwa peke yake.

Yaliyotokea baadaye yanajulikana kwa wengi.

Lakini alichokifanya Yesu, alisema Ndugu Okok-Obuoga, ni kusimama upande wa mnyonge, yule mwanamke.

Dhana ya tano alisema ni uongozi adilifu wenye maono ya mbali, visheni.

Chini ya dhana hizo mbili alisema kiongozi alipaswa kuwa na visheni, siku zote kuwa na picha kubwa mbele yake.

Na ili awaze kuwa na dhana hizo mbili, Ndugu Okok-Obuoga alisema kiongozi huyo anapaswa atoke nje ya picha, asikae ndani ya fremu ya picha kwani kufanya hivyo kutamnyima fursa ya kuiona ile picha vizuri.

Kwa kifupi, maana kamili ya dhana hizi mbili ni kwamba kiongozi hapaswi kusumbuliwa na matatizo au vitu vidogo vidogo.

Matatizo ni lazima atayapata katika utekelezaji, kwani kutokea kwa matatizo sio lazima tu bali ni sehemu ya maisha ya binadamu.

Lakini kitu kikubwa kuzingatia siku zote ni je malengo yake yataweza kufikiwa?

Akisimama nje ya fremu ya picha, ataweza kuona ni kwa namna gani angependa mabadiliko katika jamii yake.

Ndugu Okok-Obuoga alinukuu dhana hiyo ya kukaa nje ya fremu ya picha kutoka kwa mwandishi mmoja aitwaye R. S. Trapp.

Mtoa mada huyo kutoka nchini Kenya pia alizungumzia umuhimu wa kutoa taarifa yoyote ile juu ya jambo kubwa chini ya mwavuli wa uongozi wa chama chao.

Kwa mfano, tamko kuhusu msimamo wao kuhusu uchaguzi mkuu litolewe chini ya uongozi wa mashariki ya dini yote na kwa pamoja.

Amesema mtindo huu husaidia kuongeza kukubalika kwa taarifa kwa jamii kuliko kama taarifa hiyo ingetayarishwa na mashirika yote ya dini lakini ikatolewa na shirika moja la dini kwa niaba ya masharika mengine.

Ndugu Akok-Obuoga ambaye ni Mkatoliki, aliwasimulia kisa kimoja kuhusiana na urafiki wake na Mkenya mwenzake, Ndugu Musa Mwale, ambaye alikuwa Mwislamu.

Alisema urafiki wake na Ndugu Mwale ulikuwa wa karibu sana kiasi cha kwamba watu waliokuwa karibu naye wakati mwingine walifikiri Mwale alikuwa pia Mkatoliki.

Alisema hali hiyo ilijitokeza kwa sababu Ndugu Mwale alimuheshimu yeye kama binadamu mwenzake na Mkatoliki.

“Mwale hakuwa Mwislamu wa kawaida, alikuwa Mwislamu wa sala tano. Na kutokana na mapenzi yake ya kusali mara kwa mara, baada ya muda yalinifanya na mimi kusali zaidi,” Okok anasema.

Ndugu Okok alisema kuwa mwisho wa siku, Ndugu Mwale alimfanya yeye kuwa Mkatoliki zaidi.

Kutokana na hali hiyo, alisema siku moja alimwambia Ndugu Mwale kuwa alikuwa ameshindwa kumgeuza Mkatoliki.

Naye Mwale akaniambia, “Ndugu Okok, nimeshindwa kukufanya Mwislamu,” alikiri.

Kwa kifupi Ndugu Okok-Obuoga alisema hiyo ndio ilikuwa faida ya kutambua na kuheshimu kuwepo kwa tofauti zenu za dini.

Lakini badala ya kutumia tofauti hizo katika kuingiza mivutano kati yenu. Badala yake mnazitumia tofauti hizo katika kujenga uhusiano wa karibu ambao hatimaye unawasaidia katika kutatua matatizo makubwa yanayoikabili nchi yenu.

Akizungumzia kwa mara nyingine dhana ya ukweli, Ndugu Okok-Obuoga alisema Askofu mstahafu wa kanisa la Anglikan la mjini Cape Town, nchini Afrika Kusini, Desmond Tutu, wakati akiwa Mwenyekiti wa Tume ya Ukweli na Maridhiano ya Afrika Kusini katika miaka ya tisini aliwahi kusema hivi:

“Mtu mwenye kidonda akiosha kidonda chake na spiriti, kisha akaweka dawa na halafu akakifunga kidonda hicho na kitambaa, kidonda hicho kitapona haraka.

Lakini mtu huyo huyo akiamua kufunika kidonda chake na dawa bila kuosha na spirit kwa kuwa anaogopa maumivu, kidonda hicho kitaoza na hatimaye itawalazimu madaktari kukikata kiungo chake,” alisema.

Tutu alisema kadhalika hivyo ndivyo ilivyokuwa katika kusema ukweli. Ukweli wakati mwingine unauma. Lakini ukishasema ukweli, basi mtu anakuwa huru kabisa na dhamira yake inakuwa nyeupe. Hasumbuliwi tena na chochote,” Ndugu Okok-Obuoga alimnukuu Askofu Desmond Tutu akisema.

Ndugu Okok-Obuoga alisema ukweli ulimsaidia wakati mmoja kutatua mgogoro wa kidini nchini Nigeria.

Baada ya hapo, mtoa mada huyo aliwaeleza kwa kirefu jinsi Kenya ilivyojikuta ikiingia katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe baada ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Alisema yale mapigano yasingelitokea kama viongozi wa dini nchini Kenya wangelikuwa na ushirikiano tangu mwanzo.

Tatizo ni kwamba kila walipokubaliana kutokubaliana, badala ya kuendelea na mazungumzo, kila shirika la dini lilijiingiza katika biashara ya kikabila.

Kibaya kuliko vyote, alisema redio za FM nchini Kenya, kama ilivyokuwa nchini Rwanda kabla ya mauaji ya kimbari, zikajikita katika siasa za kueneza chuki miongoni mwa wananchi.

Ndugu Okok alisema kuwa mauaji yaliyotokea nchini mwao yamewafanya sio tu kuheshimiana bali kuogopa vita.

Hali hiyo, alisema hatimaye imewasaidia kuwa na katiba mpya ambayo wananchi wote walishiriki katika kuitayarisha.

Alisema kwa muda mrefu wananchi wa Kenya walikuwa wanataka kuwa na katiba mpya kwa kuwa walikuwa wanaamini kuwa ni kwa kupata katiba mpya tu ndio wangeweza kuondokana na tatizo la utawala mbaya nchini mwao.

Mtoa mada huyo alisema kushindwa kupata mapema katiba yao kwa kiasi kikubwa kulitokana na migogoro na visa mbalimbali vilivyokuwa vikifanywa na serikali ya Rais Daniel Arap Moi.

Ndugu Okok alisema kuwa baada ya kutokea kwa mapigano hayo, sasa itakuwa vigumu sana kwa mtu nchini Kenya au nje ya nchi hiyo kuwachochea watu wa Kenya kupigana.

Aliwataka viongozi wa dini wa Tanzania kuhakikisha kuwa wanazifuatia kwa karibu sana redio za FM nchini kwani katika nchi nyingine zimekuwa chanzo kikubwa cha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe.

Alisema redio za FM zikitumiwa vizuri, zitakuwa chombo kizuri sana cha kuunganisha wananchi nchini.

Ndugu Okok-Obuoga alisema wakati fulani akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu mjini Nairobi, alipigwa risasi ya mpira na polisi baada ya kujihusisha na maandamano ya kudai katiba mpya.

Alisema akiwa amelazwa hospitalini mjini Nairobi kwa matibabu, kaka yake alimshutumu sana kwa kujihusisha na siasa. Baada ya muda nilijikuta nikirudia kuwepo katika maandamano.

Katika jitihada zao za kuhakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru and wa haki, Ndugu Okok-Obuoga alisema viongozi wa dini wanapaswa pia kuchunguza kama ilani za uchaguzi za vyama vya siasa kweli zilikuwa na nia ya kuondoa matatizo nchini.

Pia aliwataka washiriki katika mkutano huo kutumia jukwaa lao la IRCPT katika kuchochea maendeleo katika nyanja mbalimbali nchini.

Kwa bahati nzuri, alisema, Tanzania ilikuwa haijapungukiwa na watu wa kuigwa kama mfano.

Kwa mfano alimtaja aliyekuwa rais wa awamu ya kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, kama mmoja wa watu ambao maisha yao yanapaswa kuigwa na wananchi wa Tanzania.

Wakati wa uhai wake, alisema Mwalimu aliwahi kusema: 'it can be done if you play your part' "inawezekana ikiwa utatekeleza wajibu wako".

Kwa hiyo mnachotakiwa kufanya sasa, alisema, ni kwa kila mmoja wenu kutimiza wajibu wake kama alivyosema baba wa taifa na mtapata mafanikio.

## 2. MAJADILIANO YA MADA YA NDUGU OKOK-OBUOGA

Ndugu Riziki Mngwali (Tanzania Women Interfaith Network) alitaka kufahamu ni kitu gani Ndugu Okok alikiona kwa viongozi wa dini wa Tanzania ambacho viongozi hao wangeweza kukitumia katika kutatua matatizo nchini.

Naye Hamisi Kassongo (Bahai Faith) alitaka kujua kama IRCPT ingeweza kutoa taarifa yoyote juu ya uchaguzi mkuu kabla ya tarehe 31, Oktoba, 2010.

Naye Pazi Mwinyimvua (Tanzania Muslimu Professionals) alidai kuwa Biblia ilisomwa na mgombea katika mkutano wa kampeni mjini Babati hivi karibuni na kwamba tukio hilo lilionyeshwa katika televisheni ya taifa, TBC.

Alisema alitegemea TEC na CCT kukemea tabia hiyo ya kuchanganya siasa na dini (chini ya msimamo wa viongozi wa dini kukaa nje ya fremu ya picha).

Lakini kwa mshangao mkubwa mashirika hayo ya dini yalikaa kimya.

Ndugu Mwinyimvua alisema kuwa tabia hiyo ikiachwa kuendelea inaweza kuwafanya waislamu nao kusoma Qu'ran kwenye mikutano ya siasa na hivyo hatimaye kulipeleka taifa pabaya.

Aliwataka Wakristu kukemea hilo na kuongeza kuwa ikiwa hivi sasa hali ndivyo ilivyo, basi hali itakuwa mbaya zaidi katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Ndugu Mwinyimvua alitoa uchambuzi wake wa hali ya siasa itakavyokuwa katika uchaguzi mkuu miaka mitano kuanzia sasa.

Alisema kutakuwa na matatizo makubwa mawili. Mosi, alisema chama cha CCM, kitakuwa katika mchakato wa kumtafuta mgombea mwingine, baada ya Rais Jakaya Kikwete kumaliza vipindi vyake viwili vya urais.

Pili, katika hilo, Wazanzibari watataka kuweka mtu wao baada ya vipindi viwili vya miaka 20 kuwa nje ya urais wa Muungano.

Lakini pia, alisema Wakristu nao watataka kuwa na mtu wao katika nafasi hiyo.

Kutokana na mivutano hiyo mikubwa miwili, Ndugu Mwinyimvua alisema suala la udini lilipaswa kuzuiwa kwa nguvu zote kwani ukiongeza na mambo hayo makubwa mawili, basi vurugu itakayotokea itakuwa kubwa sana.

Naye Hamza Mtunu (Bakwata) alidai kuwa wakati wa kile kilichojulikana kama machafuko ya Mwembechai, mjini Dar es Salaam, waislamu kadhaa waliuawa.



Lakini Wakristu walikaa kimya. Naye Abdallah Tego (Tanzania Muslim Professionals) alimpa hongera Ndugu Okok kwa mada yake nzuri.

Alisema mengi aliyoyasema Ndugu Okok ingekuwa vyema kama yangeigwa na IRCPT.

Alisema moja ya matatizo makubwa yanayoikabili Tanzania hivi sasa ilikwa ni uwoga, wasiwasi na ujinga.

Hivyo alisema kulikuwa na haja kubwa ya kutoa elimu kwa wananchi ili kuwatoa woga, wasiwasi na ujinga.

Naye Mchungaji Sistus Mallya (Pentecostal Council of Tanzania) alisema kuwa matatizo mengi yaliyokuwa yakiikabili Tanzania yalikuwa yanatokana na wananchi kutomuogopa Mwenyezi Mungu.



Alisema wakati ulikuwa umefika kwa Watanzania kumuogopa Mwenyezi Mungu.

Kwa mara nyingine tena, Mchungaji huyo akaishambulia taasisi ya Konrad Adenauer kwa kuchapisha kijitabu ambacho alidai yaliyomo ndani yake hayakuwa yanawakilisha yale yaliyozungumzwa katika mkutano kama huo uliofanyika mwaka jana mjini Dar es Salaam.

Aliendelea kudai kuwa chapisho hilo lilikuwa limewakandamiza Wakristu na kuwanyanyua Waislamu.

Na katika ngazi ya taifa, Mchungaji huyo alisema nchi ilikuwa inakabiliwa na tatizo kubwa la ukabila, utoaji ajira katika misingi ya undugu, uchu wa kutisha wa fedha na kwamba kibaya kuliko vyote ni kwamba mambo hayo yalikuwa yakiendeshwa katika ngazi ya juu ya uongozi wa kitaifa.

Aliendelea kudai kuwa kinyume na hali ya mambo ilivyokuwa katika miaka ya nyuma, ajira katika jeshi la ulinzi na sehemu nyingine nyeti ilikuwa ikiendeshwa chini ya misingi ya kujuana.

Mchungaji huyo alisema kuwa cha kushangaza ni kwamba wale waliokuwa wanadai kuwa yalitokea mauaji ya waislamu wakati wa mauaji ya Mwembechai walikuwa hawasemi chochote juu ya mauaji yaliyokuwa yakiendelea kila siku nchini ambayo alidai kuwa yalikuwa yanatekelezwa mbele ya vyombo vya dola.

Naye Ramadhani Hamisi (BAKWATA) alikuwa na haya ya kusema:

"Inawezekana kabisa, kwa yule mgombea Mkristu ilikuwa vema kwake kutumia Biblia wakati wa mkutano ule wa siasa, katika tukio linalodaiwa kuwa lilitokea mjini Babati. Lakini nina uhakika mambo yangekuwa mengine kama Mwislamu angetumia Qu'ran katika mkutano wa kampeni za kisiasa.

Kelele ambazo zingesikika zingekuwa nyingi, alisema Ndugu Hamisi.

Na ndipo Ndugu George Kanga (IRCPT) aliposimama na kusema kuwa mkutano huo ulikuwa umetoka nje ya mada yake kuu ambayo ilikuwa: 'nafasi ya mashirika ya dini katika kuhakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki.'

## 3. MAJIBU YA NDUGU OKOK-OBUOGA:

Akijibu baadhi ya maswali na maoni yaliyotolewa na washiriki, Ndugu Okok-Obuoga alisema kuwa masuala ya imani yalikuwa nyeti sana.

Akizungumzia suala la utata unaodaiwa na Mchungaji Mallya kuletwa na uchapishaji wa kijitabu na taasisi ya Konrad Adenauer, mtoa mada huyo alisema yaliyosemwa na Mchungaji huyo hayakuwa mageni katika nyanja ya dini.

Lakini alisisitiza haja ya washiriki kuwa watulivu kwa kujielekeza katika picha kubwa ya matatizo ya nchi.



Aliwauliza washiriki kuwa je ilikuwa busara kumwaga maji yaliyotumika kumuogeshea mtoto pamoja na mtoto?

Ndugu Okok alisema kadhalika suala lililoibuliwa na kijitabu hicho linapaswa kupewa mtazamo huo.

Ndugu Okok alikuwa na maana ya kusema kuwa washiriki kwenye mkutano huo walipaswa kuangalia mambo ya msingi ambayo yatawapeleka hatua moja mbele na sio kuwarudisha nyuma.

Hata hivyo mtoa mada huyo alisema kuwa kwa kusema hivyo, hakuwa na maana watu wasiseme kile wanachofikiria kuwa ni cha kweli, la hasha. Waendelea kusema tu.

Kadhalika, Ndugu Okok alisema kuwa suala la Mahakama ya Kadhi lililokuwa limejitokeza kwenye mkutano wa aina hiyo uliofanyika mwaka jana mjini Dar es Salaam halikuwa geni.

Alisema suala hilo pia liliitikisa Kenya.

Alisema nchini kwao Wakristu walionyesha kukerwa na suala hilo kiasi kwamba hawakupenda hata kulizungumzia.

Wakati fulani alisema wakristu nchini kwao walitaka suala hilo liwekwe kwenye Bunge na siyo ndani ya Katiba.

Lakini Waislamu walipinga vikali pendekezo hilo kwa madai kuwa kuwekwa kwa suala hilo kwenye Bunge siku moja lingeondolewa ikiwa idadi ya wabunge wanaopinga Mahakama ya Kadhi ingeongezeka.



Mtoa mada huyo alisema yeye binafsi aliwauliza wanasheria Wakristu ikiwa kinga ya namna fulani ingewekwa kuzuia suala la Kadhi kutoondolewa kwenye sheria ya Bunge, kama hilo lingekubalika kwao?.

Ndugu Okok alisema wanasheria walimjibu kuwa hilo halingekuwa na tatizo.

Kwa hiyo walipokubali kuwekwa kwa sheria hiyo ya kinga, tatizo la Mahakama ya Kadhi likawa limepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mtoa mada huyo alisema mbinu kama hiyo iliyotumika kutatua suala la Mahakama ya Kadhi nchini Kenya ingeweza kutumiwa nchini Tanzania katika kutatua masuala nyeti ya imani ambayo yalikuwa yanaikabili nchi.

Lakini alisema hilo linawezekana tu ikiwa viongozi wa dini chini ya jukwaa la IRCPT watajenga utamaduni wa kuwa na mawasiliano na mazungumzo ya mara kwa mara.

Akizungumzia suala la matumizi ya Biblia kwenye mkutano wa kampeni za kisiasa, Ndugu Okok alisema: "kama kweli hilo lilitokea katika namna tulivyoelezwa, basi hilo ni tatizo."

Hata hivyo mtoa mada huyo alisema masuala ya aina hiyo yanayojikita katika utoaji wa taarifa wa matukio yaliyotokea pia yanategemea yameelezwa vipi.

Inawezekana kabisa matumizi ya Biblia hiyo hayakuwa na nia ya kuuinua Ukristu, pengine ulikwa ni mfano tu wa jinsi dini moja ilivyokuwa ikiangalia tatizo fulani.

Ndugu Okok alitahadharisha haja ya kuwa waangalifu wanapozungumzia masuala nyeti ya imani.

Baada ya hapo na kuhusiana na hilo akaeleza kisa kilichotokea katika hoteli moja maarufu mjini Morogoro ijulikanayo kwa jina la Hotel 88.

Alisema alikuwa ametakiwa kutoa mada kwa vijana juu ya namna ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa ukimwi.

Lakini kabla ya kutoa mada hiyo, alitahadharishwa na wenzeke, kuwa kulikuwa na kikundi kikubwa cha vijana wa kiislamu nje ya hoteli hiyo.

Kufuatana na taarifa hiyo, kama angezungumzia matumizi ya kondomu kama kinga dhidi ya ugonjwa huo, basi kungekuwa na tatizo.

Tatizo la vijana wale, anasema Ndugu Okok-Obuoga, ni kwamba hawakujua kuwa alikuwa na uzoefu mkubwa katika mada za namna ile.

Isitoshe, alisema alikuwa ametoa mada za namna hiyo kwenye nchi kama vile Senegal na Sierra Leone, nchi ambazo alisema zilikuwa na idadi kubwa ya waislamu na tena wenye msimamo mkali. Lakini sikupata tatizo lolote.

Jambo jingeni ambalo alikuwa ameelezwa ni kwamba ndani ya chumba kile cha mkutano, kulikuwa na washiriki halali kabisa lakini ambao moja ya kazi yao ilikuwa kumsikiliza mtoa mada kwa makini na kwamba kama angejihusisha na suala la kondomu, basi kazi yao ilikuwa kutoa taarifa kwa vijana waliokuwa nje ya hoteli ile.

Wakati wa kutoa mada ulipowadia, Ndugu Okok-Obuoga anasema vijana kama wawili walianza kumkabili kwa maswali kwa namna iliyoashiria kuwepo kwa kile alichokuwa amekwishaambiwa.

“Nilianza kwa kumuuliza mmoja wa vijana hao kama dini yake ya kiislamu ilikuwa inamruhusu kufanya mapenzi katika umri wake huo mdogo, naye akanijibu kuwa ilikuwa haimruhusu.

Na hapo ndipo nilipomwambia kuwa kwa kuwa dini yake ilikuwa haimruhusu, basi hakutakiwa kutumia kinga ya aina yoyote ile kwa sababu hatakiwi kabisa kufanya mapenzi na mwanamke katika umri ule.

Mtoa mada huyo anaendelea na kusema likaja suala la wale waliokwishaoa.

Aliwauliza watu hao kama walikuwa wanaruhusiwa kufanya mapenzi na wanawake ambao sio wake zao.

Kadhalika, anasema, walimjibu kuwa walikuwa hawaruhusiwi.

“Basi ikiwa ni hivyo,” akaendelea, “kwanini utumie kinga dhidi ya mwanamke ambaye sio mkeo.

Kwanini usijizuie kufanya mapenzi na mwanamke huyo kama unavyoongozwa bayana na dini yako,” aliuliza.

Mwisho wa siku anasema alifanikiwa kuonyesha kuwa mtu anaweza kujikinga na maambukizi ya ukimwi kwa kutumia mafundisho ya imani na muongozo wa dini yake na siyo kondomu.

Siku ya pili, anasema Ndugu Okok, chumba cha mkutano kilijaa zaidi.

Kwani karibu vijana wote waliokuwa nje walikuwa wanataka kuhudhuria mkutano ule baada ya kupata taarifa kwa wenzao kuwa kinyume cha walivyokuwa wameambiwa hapo awali, mtoa mada huyo alikuwa na habari njema ambazo zilikuwa kwa namna fulani zinafanana na mafundisho ya dini yao.

Aliwaambia viongozi hao wa dini kuwa ili wao waweze pia kufanikiwa, walipaswa kuimarisha muundo wa IRCPT.

Alisema kushughulikia muundo wa IRCPT utawasaidia kama ulivyowasaidia wao katika Baraza la Afrika la Viongozi wa Dini, ACRL.

“Kwa mfano katika ACRL-RfP (dini kwa amani) visheni na malengo yanasimamiwa na viongozi wa juu ambao hutoa maelekezo chini kwenye jumuiya juu ya utekelezaji wa masuala mbalimbali,” alisema.

Kwa maana hiyo, ACRL-RfP inasimamia uandaaji wa sera, uchukuaji wa maamuzi na mipango mizima ya namna ya kushirikiana na wadau.

Hata hivyo alisistiza juu ya haja ya IRCPT kuhakikisha kuwa chochote kile kinachotakiwa kutekelezwa ni wajibu wa jukwaa hilo.

Alisema mfumo wa uendeshaji wao unahusisha utambuzi wa matatizo na namna ya kuyashughulikia.

Ndugu Abdallah Tego alisema kuwa hivi karibuni kumekuwa na malalamiko dhidi ya serikali ya Rais Kikwete juu ya uteuzi wake wa baraza la mawaziri na viongozi wengine wa ngazi za juu serikalini na mashirika ya umma.

Alisema kuwa hali hiyo ilikuwepo pia wakati wa awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere. Viongozi wengi serikalini, alisema walikuwa wakristu.

Kwa mfano nafasi nyeti kwenye baraza la mawaziri kama vile ulinzi, fedha, mambo ya kigeni na kadhalika zilishikiliwa na wakristu.

Lakini anasema wakati huo waislamu hawakulalamika.

Baada ya Ndugu Tego kumaliza, ndipo Ndugu Kassala aliposema kuwa alikuwa karibu aondoke kwenye mkutano huo. Sababu? Baada ya kugundua kuwa washiriki katika mkutano huo walikuwa wanaendelea kutoka nje ya mada iliyowaleta-jinsi mashirika ya dini yanavyoweza kusaidia kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki.

Alisema jambo la kwanza lilikuwa kuhakikisha kuwa wagombea na wapiga kura wote wanahusishwa na zoezi zima la uchaguzi. Kwa mafano, Ndugu Kassala alisisitiza kuwa huwezi kutenganisha maadili na uongozi.

Alisema mtu yoyote anayetaka kuchaguliwa kiongozi, kwanza anatakiwa kutimiza masuala yote yanayohusiana na maadili.

Kwa kifupi mtu huyo anatakiwa kuwa mwadilifu kufuatana na imani zetu za dini.



Alisema kulikuwa na haja pia ya kuhakikisha kuwa maadili yanazingatiwa katika michakato yote ya uchaguzi.

Kutoka uteuzi wa wagombea katika kila chama mpaka kwenye uandikishaji wa wapiga kura, upigaji wa kura, kuhesabu kura na hatimaye katika kutoa matokeo ya washindi na walioshindwa.

Hatua zote hizo zinapaswa kuzingatia maadili, alisistiza.

Kwa bahati mbaya alisema mambo ambayo wamekuwa wakiyasoma, wakiyasikia na kuyaona kupitia vyombo vya habari- magazeti, redio na runinga, yalikuwa yanatoa picha mbaya sana.

Vyombo vya habari vimeonyesha kuwepo kwa ukabila, udini, ufisadi, rushwa, uchochezi na matukio kadhaa ya uvunjifu wa haki za binadamu.

Akasema: "kama tunafikiri vitu ambavyo tumekuwa tukivisoma, kusikia na kuona ni vibaya, basi tuna wajibu wa kusema hivyo. Lakini hiyo haitoshi," alisema na kuendelea, "tunapaswa pia kupanga mkakati wa namna ya kutatua matatizo hayo," alisisitiza.

Kwa bahati nzuri, alisema kuwa Watanzania walikuwa na wimbo wa taifa ambao ulikuwa unasema kuwa ngao zao dhidi ya maadui zilikuwa hekima, amani na umoja.

Alisema kwa muda mrefu uamuzi wa Watanzania kutegemea hekima, amani na umoja kama ngao dhidi ya maadui wao, ulikuwa umewawezesha kuwa na amani nchini.

Lakini alisema kwa bahati mbaya, katika siku za hivi karibuni, baadhi ya Watanzania wameyumba.

Hili amesema limetokana na kutafuta na kukumbatia ngao zisizofaa!

Ndugu Kassala amezitaja ngao hizo zisizofaa kama vile fedha, ufisadi, rushwa, ukabila na ujenzi wa matabaka.

Alisema kitu kingine kilichosaidia Tanzania kuwa na amani katika miaka ya nyuma ni msimamo wa kitaifa wenye kuzingatia haki za binadamu.

Kwa hiyo viongozi wa dini wanapoliangalia suala zima la kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki, basi inapaswa kuzingatia mambo hayo mawili, yale yaliyomo kwenye wimbo wa taifa na uzingatiaji wa haki za binadamu.

Akitoa mchango wake wakati wa majadiliano, Katibu Mkuu wa IRCPT, Ndugu Omari alisema alikuwa anasikitishwa juu ya kushindwa kwa baadhi ya vyama vya upinzani kujitayarisha vizuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kwa mfano alisema lilikuwa jambo la kusikitisha kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Chadema, kuingia kwenye mchakato wa uchaguzi na asilimia 75 tu ya wagombea wa viti vya ubunge.

Hii ina maana ya kuwa Chadema tayari wamekwishapoteza asilimia 25 ya viti vya ubunge hata kabla ya zoezi la kupiga kura halijaanza!

Alisema isitoshe, chama hicho kimeanza kuvuma wakati wa mchakato, na hili Katibu Mkuu huyo analiona litakuja kuwa tatizo kubwa baadaye ikiwa chama kitafanya vibaya.

Naye Ndugu Steven Andrew (TADIP) alisema kulikuwa na haja kubwa kwa mashirika ya dini kutambua nafasi yao katika kuhakiksha uchaguzi mkuu unakuwa huru na wa haki.

Alisema wakati ulikuwa umefika kwa jukwaa kama vile IRCPT kuchunguza ushawishi wake katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Kwa mfano, alisema moja ya maswali jukwaa hilo linapaswa kujiuliza ni matamko yake mangapi yametekelezwa.

Au ni kwa namana gani IRCPT limekuwa likijihusisha na mchakato wa kuishawishi serikali kuanzisha mchakato wa kutayarisha katiba mpya ya nchi.

Alisema lilikuwa ni suala lisilopingika kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi haikuwa huru, hii ni kutokana na uwajibikaji na uteuzi wa wafanyakazi wa tume hiyo.

Na kutokana na hilo, alisema kulikuwa na haja ya kuanzisha mchakato, kupitia vikao halali, utakaopelekea kuishawishi serikali kuundwa kwa tume huru.

Alisema kama IRCPT inafikiria ilikuwa na uwezo wa kushughulikia hayo niliyoyataja, basi ianze kazi hiyo na kamwe isiyumbe.

Kwa upande mwingine, Ndugu Imelda Maboya (Pentecostal Council of Tanzania) alisema ni ndoto kufikiria kuwa Tanzania itakuwa na uchaguzi huru na wa haki kwa kutumia katiba iliyopitwa na wakati.

Alisisitiza kuwa uchaguzi huru na wa haki unaweza tu kupatikana chini ya katiba iliyotayarishwa kwa ajili hiyo.

Hata hivyo, kwa hili alisema mashirika ya dini yana mchango mkubwa, kwani kwanza yanao wafuasi wengi ambao ndio pia wapiga kura.

Alisema ikiwa serikali iliyoko madarakani haiko tayari kuendesha elimu ya uraia, basi viongozi wa dini kupitia jukwaa lao la IRCPT wanapaswa kuchukua fursa hiyo.

Alisema baada ya kuwasikiliza washiriki katika mkutano huo, aligundua kuwa tatizo sio dini au tofauti zake.

Bali kama wale waliokuwa wanawaongoza, viongozi hao walikuwa wamechoka na kukatishwa tamaa na viongozi wao wa siasa na mfumo wa uongozi huo hapa nchini.

“Kwa mfano fikiria hili,” alisema na kukaa kimya kwa muda- “Inawezekanaje watuhumiwa na wahalifu wakaruhusiwa kugombea nafasi za uongozi wa juu nchini. Je hili linaingia akilini” aliuliza.

Naye Ndugu Frederick Bomani (CETA) alisema haoni kama pana haki katika uwanja wa uchaguzi na hivyo kwake yeye kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki kwa muda huu itakuwa ni ndoto tu.

Ndugu Bomani akauliza juu ya uwezekano wa viongozi wa dini kuwa waangalizi na wafuatiliaji wa uchaguzi mkuu huu.

Alisema hakuna kitu kilichoonesha matatizo makubwa yanayoikabili nyanja ya uchaguzi mkuu nchini zaidi ya mchakato mzima wa uteuzi wa viongozi ndani ya chama.

Alitoa mfano wa wagombea tisa, wanane walikuwa na shahada za chuo kikuu na mmoja alikuwa na elimu ya darasa la saba.

Kwa mshangao wa kila mtu, anasema Ndudu Bomani ulipokuja wakati wa uteuzi, watu wanane waliokuwa na shahada za chuo kikuu waliachwa na yule wa darasa la saba akateuliwa kugombea ubunge.

Cha kusikitisha zaidi, alisema, elimu ya uraia ililetwa ikiwa umebaki muda mchache sana kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Katika kujadili hoja ya washiriki, Mchungaji Mallya ambaye aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanashiriki katika uchaguzi mkuu kama waangalizi na wafuatiliaji.

Pia aliwataka washiriki wenzake kuanza kufikiria namna ya kupata fedha kwa ajili ya kuendeshea jukuwaa lao la IRCPT.

Kwa mfano alisema hata mkutano wa siku tatu ambao ulikuwa unafikia ukingoni. ulikuwa umefadhiliwa na taasisi ya nje ya nchi.


Mchungaji Mallya alisema hiyo ni  moja ya changamoto zinazotukabili viongozi wa dini.

**SEHEMU C:**

## UWASILISHAJI WA MADA JUU YA WAJIBU WA MASHARIKA YA DINI KATIKA KUHAKIKISHA UWEPO WA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI

### 1. MADA YA PILI: NAFASI YA MASHIRIKA YA DINI KATIKA UCHAGUZI HURU NA WA HAKI; Ndugu Ebenezer Mshana.

Siku ya pili ya mkutano wa Wawakilishi wa Mashirika ya dini nchini Tanzania, IRCPT, ilianza kwa uwasilishaji wa mada na Mhadhiri wa Chuo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndugu Ebenezer Mshana.




Katika mada yake aliyoipa jina ***la Nafasi ya Mashirika ya Dini katika kuhakikisha Kuwepo kwa Uchaguzi Huru na wa Haki,*** Ndugu Mshana aliigawanya mada hii katika sehemu kuu mbili.

Katika sehemu ya kwanza, Ndugu Mshana aliangalia kwa undani nini maana ya uchauguzi huru na wa haki.

Sehemu ya pili, mhadhiri huyo aliangalia nini nafasi ya mashirika ya dini katika kuhakikisha kuwa dhana nzima ya uchaguzi huru na wa haki inatekelezwa.

Ndugu Mshana alisema wananchi wengi nchini Tanzania walikuwa waumini wa dini mbalimbali.

Alisema takwimu zilikuwa zinaonesha kuwa karibu theluthi mbili ya watu zaidi ya millioni 40 walikuwa waumini wa dini rasmi.

Alisema mbali na kutoa muongozo katika masuala ya imani, dini nchini Tanzania zilikuwa zikitoa mchango mkubwa katika huduma za afya na elimu.

Kwa kifupi, alisema utoaji wa huduma hizo tatu za imani, afya na elimu zimezisaidia dini kujipatia ufuasi mkubwa wa wananchi.

Alisema ushawishi mkubwa wa dini mbalimbali nchini Tanzania ukitumiwa vizuri na dini hizo unaweza kuleta maendeleo makubwa katika suala zima la kujenga umoja na ushirikiano na hivyo kuendeleza amani na utulivu nchini.

Lakini alionya kuwa ushawishi huo ukitumiwa vibaya, basi dini zinaweza kuwa vyombo vikubwa vya kueneza chuki, na hivyo uadui miongoni mwa wananchi jambo ambalo ni dhahiri litapelekea kuvurugika amani na utulivu nchini.

Alitoa mfano wa jinsi dini zilivyosaidia kuleta mfarakano barani Afrika kama vile katika nchi jirani ya Rwanda ambako zaidi ya watu laki nane wa kabila dogo la watutsi na wahutu wa mlengo wa kati walipouawa katika mauaji ya kimbari mwaka 1994.

Alisema uhuru wa kuabudu nchini Tanzania ulikuwa unasimamiwa na kifungu 19 (2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambacho kinasema: "Bila kuathiri sheria zinazohusika za Jamhuri ya Muungano, kazi za kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiari ya mtu binafsi, na shughuli za uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli ya Mamlaka ya Nchi."

Mwaka 1992 uamuzi ulipofikiwa wa kuingia katika mfumo wa vyama vingi, katiba ya nchi haikuandikwa upya.

Badala yake ilifanyiwa mabadiliko kidogo ya hapa na pale.

Kubwa, lilikuwa ni  kuweka miiko kwa vyama vya siasa, miiko ambayo ilikuwa na lengo la kuendelea kujenga na kuimarisha uhuru, umoja na amani nchini.

Kadhalika, sera ya Ujamaa na Kujitegemea haikuguswa. Ijapokuwa katika utekelezaji, mambo yalikuwa tofauti, kwani ni ukweli usiopingika kuwa sera inayotekelezwa sasa katika nyanja ya uchumi ni soko huria.

Baadhi ya miiko iliyowekwa kwa vyama vya siasa na imekuwa ikitekelezwa mpaka sasa ni nyumba za ibada kutotumika katika siasa, kutotumia ukabila, udini, ubaguzi wa rangi, umajimbo na uwana taaluma katika kubagua watu kisiasa.

Mbali na kuzitaja sheria za ndani ambazo zilikuwa zinampa Mtanzania fursa na uhuru wa kujihusisha na siasa, Ndugu Mshana pia aliangalia sheria za kimataifa.

Kwa mfano, aliangalia kwa kifupi, sheria ya Umoja wa Mataifa ya 1948 inayosimamia haki ya kila mtu anayetimizia umri wa mtu mzima (kwa Tanzania ni miaka 18) kwa kuweza kuwa mgombea katika nafasi ya uongozi na kupiga kura.

Msisitizo umewekwa katika sheria hiyo ya kimataifa ya mwaka 1948 juu ya haja ya kuwepo kwa kituo cha kupigia kura ambacho mfumo wake mzima uhakikishe kuwepo kwa upigaji kura wa siri.

Ndugu Mshana pia aliangalia sheria za kimkoa kama zile zilizoko chini ya nchi za kusini mwa Afrika, SADC.

Kimataifa, alisema sheria hizo zilikuwa chini ya sheria ya kimataifa ya haki na kisiasa ya mwaka 1966 ambayo ilikuwa imetoa matamko yafuatayo:

Kwamba mbali ya wananchi kuhakikishiwa uhuru, pia wawe huru kuitisha mikutano, kukusanyika, kwenda kokote nchini mwao ili mradi tu hawavunji sheria za nchi na kuhakikishiwa uhuru wa kuongea.

Katika suala zima la uhuru wa kuongea, Ndugu Mshana alisisitiza haja, hasa wakati wa kampeni za siasa na uchaguzi kama ilivyo hivi sasa, kwa wahusika kutotumia lugha za matusi.

Chini ya sheria za ndani, za kimkoa na kimataifa, Ndugu Mshana alisema serikali ilikuwa inasisitiziwa kuhakikisha kuwa wagombea wote wanapewa haki sawa katika matumizi ya rasilimali za nchi katika kampeni zao.

Haki hiyo, alisema ilikuwa pia inajumuisha matumizi ya vyombo vya habari, hasa vile vinavyomilikiwa na serikali (na hivyo kuendeshwa na fedha za walipa kodi) kutoa nafasi sawa kwa wagombea wa vyama vyote vya siasa katika kujitangaza.

Katika ngazi ya Afrika, Ndugu Mshana alizungumzia juu ya yale yaliyomo katika mkataba wa Afrika na mambo ambayo mkataba huo wa kisheria ulikuwa unazitaka nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania, zitekeleze.

Kadhalika, alisema SADC pia ilikuwa na msisitizo wake kuhusiana na yale ambayo jumuiya hiyo ilizitaka nchi wanachama kutekeleza katika kuhakikisha kuwepo kwa mazingira huru na ya haki kwa mwananchi katika ushiriki wake katika suala zima la uchaguzi.

Ndugu Mshana alizitaja sifa ambazo zilikuwa zinatakiwa kutekelezwa kwa uchaguzi huru na haki.

Ni sifa zifuatazo:

1. Kutokuwepo kwa aina yoyote ile ya vitisho kwa wapiga kura au wagombea-kwa maneno au vitendo,

2. Kuwepo kwa mfumo mzuri wa vituo vya kupigia kura kwa maana ya kuhakikisha usiri katika upigaji wa kura,

3. Zoezi la upigaji kura liwe la siri,

4. Kuhesabu kura zilizopigwa kuwe kwa uwazi,

5. Kuwepo kwa vyombo vya usimamizi wa zoezi hilo ambavyo havifungamani na upande wowote, viwe huru, vinavyozingatia haki na mojawapo ikiwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, NEC,

6. Kuwepo kwa mfumo wa haki wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa. Mbali na kuzingatia miiko iliyowekwa kwa vyama vya siasa, vyama hivyo pia vinapaswa kuhakikisha uteuzi huo haujihusishi kwa namna yoyote ile na vitendo vya rushwa,

7. Uwepo wa vyombo vya habari, hasa vile vinavyomilikiwa na umma, visivyofungamana na upande wowote, vyombo ambavyo pia vinazingatia haki katika kutangaza habari za wagombea na sera za vyama vyao,

8. Mgawanyo sawa wa matumizi ya rasimali ya taifa kwa vyama vyote vya kisiasa kabla na wakati wa kampeni za uchaguzi,

9. Kutojihusisha na chama chochote cha siasa kwa wafanyakazi serikalini na vyombo vya umma.

Ndugu Mshana alisisitiza kuwa uchaguzi huru na wa haki unaanzia kutoka kwenye uandikishaji wa wapiga kura mpaka uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa. Na kutoka zoezi la upigaji wa kura mpaka kwenye hatua ya

kuhesabu kura zilizopigwa, na hatimaye, kutangaza washindi na walioshindwa katika nafasi mbalimbali.

Hata hivyo Ndugu Mshana alisema kuwa utafiti wa haraka haraka ulikuwa unaonesha kuwa ilikuwa vigumu sana kuhakikisha utekelezaji wa vigezo vinavyohakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki.

Kwa mfano alisema tokea uchaguzi wa kwanza chini ya mfumo wa vyama vingi wa mwaka 1995 mpaka mwaka 2005, kumekuwa na matatizo mengi ambayo yamefanya chaguzi hizo kukosa sifa za chaguzi huru na haki.

Ameyataja matatizo hayo kama vile kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa kidemokrasia katika zoezi zima la uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, vyombo vya habari vinavyofungamana na vyama vya siasa na hasa chama tawala, na kuendelea kuwepo kwa wafanyakazi wa serikali ambao wanaonyesha mapenzi yao kwa vitendo kwa chama tawala.

Aliyataja matatizo mengine kama vile kuwepo kwa vitisho dhidi ya mgombea mmoja mmoja na vyama vyao na wananchi wote kwa ujumla, kujipenyeza kwa siasa za ukabila, umajimbo, udini na ubaguzi wa rangi.

Ndugu Mshana alisema mashirika ya dini yanao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa uchaguzi nchini unaendeshwa chini ya misingi huru na ya haki.

Alitaja baadhi ya vitu ambavyo mashirika ya dini yangeweza kufanya kuhakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki kama vile kuendesha elimu ya uraia nchini na hivyo kuisaidia Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kazi hiyo.

Ilibainika kuwa, ijapokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilikuwa imeteuliwa, kisheria, kusimamia na kuendesha elimu ya uraia hapa nchini. pia mtu yeyote, wakiwemo viogozi wa mashirika ya dini chini ya IRCPT wanaruhusiwa kuendesha elimu hiyo ya uraia baada ya kupata ruhusa kutoka na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Ndugu Mshana alitaja michango mingine ambayo inaweza kufanywa na viongozi hao wa mashirika ya dini kama vile wafuatiliaji (monitors) na waangalizi (observers) wa uchaguzi mkuu.

Alisema ijapokuwa elimu ya uraia hivi sasa ilikuwa ikitolewa mashuleni, hata hivyo kulikuwa na haja kubwa kwa elimu hiyo kutolewa pia kwa watu wazima, hasa vijijini.

Ndugu Mshana alisema kutolewa kwa elimu ya uraia kwa nchi nzima na kwa muda wa kutosha kungesaidia sana katika kuwawezesha wananchi kuchagua viongozi bora na wanaofaa.

Lakini kuendelea kwa hali ya sasa, ambapo wananchi walio wengi hawana hata elimu ya msingi ya uraia, alisema kulikuwa kunapelekea kuwepo kwa kile alichokiileza kuwa hali ya ujinga na kuendeleza upigaji wa kura bila tija.

"Hawa watu wanachagua nini hali ya kuwa zoezi la kupiga kura hawalielewi?" Ndugu Mshana aliuliza.

Pia jambo la aibu kwa taifa kama Tanzania kuendelea kutegemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje katika kugharamia elimu ya uraia kwa wananchi wake.

Hakika kuendelea, kwa Tanzania, kutegemea wafadhili kutoka nje katika kugharamia masuala yanayohusiana na viongozi gani tunataka tuwachague na tunataka tuongozwe vipi, ilikuwa inakwenda kinyume kabisa na malengo ya uhuru wa Tanganyika uliopatikana tarehe 9, Desemba mwaka 1961 na Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12, January, mwaka 1964.

Tafsiri ya hili ni kwamba kama waasisi wa mataifa yetu mawili wangekuwa wametegemea wafadhili kutoka nje kuwapa watu wao elimu ya uraia ya kujitawala, basi nchi hizi mbili hazingekuwepo hapa zilipo leo.

Mbali na kuboresha demokrasia nchini, Ndugu Mshana alibainisha kuwa uchaguzi huru na wa haki unaondoa uwezekano wa kutokea mapigano na mivutano mingine ya kisiasa mara baada ya kufanyika kwa uchaguzi.

Ndugu Mshana alitaja faida zingine za uchaguzi huru na wa haki kama kuwepo kwa amani na utulivu wa kisiasa, mambo ambayo husaidia katika kujenga uchumi imara wa nchi.

Uchaguzi huru na wa haki, husaidia katika kusimamia zoezi la ubadilishanaji wa madaraka kutoka uongozi mmoja hadi uongozi mwingine, mithili ya wanariadha wanapopokezana vijiti katika mbio za mita 100.

## 2. MAJADILIANO JUU YA MADA YA NDUGU MSHANA:

Ndugu Camillus kassala (CPT/TEC) alisema kwa kuwa Ndugu Mshana mada yake ilikuwa ya kisomi, basi kulikuwa na haja kubwa kwa viongozi wa dini kuweka vionjo vya kiimani kwa kufanya kile alichokisema viongozi hao walikuwa

wanakifahamu zaidi, ambao ni kusali na kufunga ili kumuomba Mwenyezi Mungu atoe baraka zake ili Watanzania waweze kuwa sio tu na uchaguzi huru na wa haki, bali pia wenye amani.

Alisema katika chaguzi zilizopita, Tanzania ilikuwa na tabia ya kufanya sala kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu kuiongoza nchi kuwa na uchaguzi mzuri.

"Tunasoma katika vitabu vitakatifu kuwa Yesu Kristu alisali na kufunga… ninafahamu dini nyingi hapa nchini ambazo hazina ugeni wowote katika suala zima la kusali na kufunga," alisema.

*Ndugu Kassala* pia alizungumzia haja ya kuweka msisitizo katika suala zima la kuzingatia maadili hasa katika kuwachagua viongozi bora.

Alisema viongozi wa dini nchini wana wajibu sio tu wa kuwataka waumini wao kujitokeza kwa wingi kupiga kura, bali pia kuhakikisha kuwa wanawachagua viongozi waadilifu.

*Ndugu Kassala* alisema mbali na kutoa ushauri kwa waandaaji na wasimamizi wa zoezi zima la uchaguzi na upigaji kura, viongozi wa dini pia wanawajibu mkubwa wa kuwakemea watendaji wasio waadilifu.

Alisema historia ilionyesha kuwa viongozi wa zamani wa kidini walifanya yale ambayo viongozi wa dini nchini Tanzania sasa walikuwa wanatakiwa kufanya ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa na amani na kupata viongozi wa kisiasa walio na maadili.

Ndugu Kassala alitoa mfano wa viongozi hao kama vile kiongozi wa kupigania haki nchini Marekani, Ndugu Martin Luther King Jr, Chifu Albert Luthuli na Askofu mstahafa wa Kanisa la Anglikan la Cape Town, Desmond Tutu, wote wa Afrika kusini na Mahtma Gandhi wa India.

*Mchungaji Sistus Mallya* (Pentecotal Council of Tanzania) alidai kuwa yaliyokuwa yameandikwa katika kijitabu kilichochapishwa na taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung chini ya kichwa kisemacho: ***'Wajibu wa Mashirika ya Dini katika Utawala Bora'*** yalikuwa hayawakilishi yale yote yaliyozungumzwa katika mkutano uliopita wa viongozi wa dini ambapo yeye alikuwa mmoja wa waliohudhuria.

Hii ilikuwa mara ya pili kwa Mchungaji Mallya kusema haya.

Mwezeshaji, Ndugu Salim Zagar, alimudu hali hiyo na kuwezesha majadiliano kuendelea.

Ndugu Hamisi Kassongo (Bahai Faith) katika kuchangia mjadala huo alisema ipo haja ya kuwa na mfumo wa aina moja kwa nchi nzima kutoa elimu ya uraia.



Pili, alizungumzia haja ya kuwa na mafunzo kwa ajili ya walimu ambao hatimaye wangetumiwa katika kufundisha elimu ya uraia nchini.

Naye Ndugu Pazi Mwinyimvua (Tanzania Muslim Professionals) alikuwa na mengi yafuatayo:.

Kwa mfano alionesha wazi kutofurahishwa kwake na kushindwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kushirikisha viongozi wa dini katika suala zima la uchapishaji wa makaratasi ya kupigia kura.

Akisisitiza ya Ndugu Kassongo, katika haja ya kuandaliwa kwa mfumo wa aina moja wa ufundishaji nchini wa elimu ya uraia.

Pia alitaka kufahamu maana ya maneno mawili, ufuatiliaji (monitoring) na uangalizi (observer) wakati wa uchaguzi mkuu.

Jambo la mwisho alitaka kujua faida ya kuwepo kwa serikali ya mseto kama mfumo uliokubaliwa miezi michache iliyopita Visiwani Zanzibar.

Mchango wa Ndugu Imelda Maboya (Pentecostal Council of Tanzania) ulikuwa katika mfumo wa mawazo yake zaidi kuliko swali.

Ndugu Imelda Maboya (PCT) alisema mtu akisikiliza kwa makini matamko mbalimbali ya wananchi, hasa kuhusiana na uchaguzi mkuu ujao, ilikuwa dhahiri kuwa walikuwa wanataka kuchaguliwa kwa viongozi makini.

Naye Katibu Mkuu wa IRCPT, Ndugu Ayoob Omar aliangalia, kwa mara nyingine, suala zima la miiko ya vyama vya siasa nchini.

Alionya kuwa ikiwa viongozi wa dini hawatakuwa makini wanaweza kujikuta majumba yao ya ibada yakitumiwa kwa shughuli za kisiasa.

Mchungaji Mallya (Pentescotal Council of Tanzania) alitaka kujua nafasi ya Jeshi la Wananchi la Tanzania, JWTZ, hasa kuhusiana na uchaguzi mkuu.

Alionyesha wazi kukerwa kwake na tamko lililotolewa na Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Abdulrahman Shimbo ambaye alionya kuwa jeshi lilikuwa tayari kupambana na yeyote ambaye angeleta vurugu wakati wa uchaguzi mkuu.

Mchungaji huyo pia alidai kuwa taasisi yake ya dini mara kwa mara ilikuwa inanyimwa mafunzo yaliyokuwa yanaandaliwa kwa ajili ya elimu ya uraia.

Jambo lingine ambalo alionyesha kukerwa nalo lilikuwa kuitwa kwa taasisi yake ya dini kama ni taasisi ndogo.

Alisema taasisi ambazo zilikuwa zikiidharau taasisi yake ya dini zilikuwa zile ambazo zilikuwa zikijiona kuwa ni taasisi kubwa za dini.

Alisisistiza kuwa alikuwa anakerwa sana na hilo na kwamba angependa taasisi hizo za kidini kuacha tabia hiyo mara moja.

“Hivi ukubwa na udogo wa dini unaanza na kuishia wapi?” aliuliza na kuendelea “dini zinazojiita kubwa zinapaswa kufahamu kuwa wakati fulani dini hizo zilikuwa ndogo.”

Naye Ndugu Ephraim Mkenda (TEC) alikuja na suala tofauti kabisa na hivyo kuwafanya wenzake kujaribu kutafuta maana ya alichokuwa amekisema katika kamusi zilizoko katika ubongo vichwani mwao.

Ndugu Mkenda alidai kuwa kwa muda mrefu, Watanzania wamekuwa wakipiga kura lakini wamekuwa hawachagui viongozi wao.

Alidai kuwa viongozi wa Tanzania wanachaguliwa na vyombo vingine na sio wapigaji kura. Alifafanua kwa kusema kuwa kuchagua kiongozi kwa kupiga kura maana yake ni kumpigia kura mtu unayemtaka na hatimaye kumpata.

"Kwa bahati mbaya, hiki siyo ambacho kimekuwa kikifanyika katika chaguzi nchini Tanzania.

Kuna vyombo vingine kabisa, ambavyo vimekuwa vikituchagulia viongozi hapa nchini kwa kifupi, tumekuwa tukipiga kura, hatuchagui," alisisitiza.

Mshiriki mwingine aliwasilisha swali lake ambalo linaweza kufananishwa na mfupa uliomshinda fisi pamoja na mapenzi ya mnyama huyo katika kutafuna mifupa.

Akihoji mantiki ya kura za rais kutohojiwa kisheria, aliuliza kitu gani kinaweza kutokea ikiwa uchaguzi utatangazwa kuwa haukuwa huru na wa haki.

Je matokeo ya kura za rais yatabakia kama yalivyo?

Mshiriki huyo aliendelea kusema kuwa alikuwa na ushahidi wa kutosha kuwa mfumo mzima wa serikali na chama tawala ulikuwa hautaki kutolewa nchini kwa elimu ya uraia.

"Kwa kifupi ningependa kusema hivi, mfumo mzima wa nchi ungependa wananchi waendelee kuwa mbumbumbu ili chama tawala kiendelee kuwatawala," alisema.

Alisema alikuwa na uhakika kwa yale aliyokuwa anayasema kwa kuwa ameona kwa macho yake katika maeneo mbalimbali ya vijijini aliyotembelea nchini jinsi serikali katika maeneo hayo zinavyopiga vita kuenezwa kwa elimu ya uraia.

"Ukiiambia serikali mikoani kuwa ulikuwa unataka kufundisha wananchi wa eneo hilo elimu ya uraia, wanakujibu kwa kejeli, ukishafanya hivyo, unatarajia kuvuna nini?" alisema.

Anasema amekuwa akikutana na wakuu wa wilaya ambao amesema wamekuwa na tabia ya kuwatisha watu wote ambao wanaonesha nia ya kutaka kuwafundisha wananchi elimu ya uraia.

Mshiriki huyo hakuishia hapo. Alilishutumu Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, UNDP, lenye ofisi yake mjini Dar es Salaam kwa kudai kuwa shirika hilo lilikuwa na ajenda ya siri dhidi ya Tanzania.

Alihoji kuwa kama shirika hilo halikuwa na ajenda ya siri dhidi ya Tanzania, kwanini lilikalia fedha mpaka karibu na uchaguzi mkuu?

Alisema shirika hilo liliamua kutoa fedha zinazohusiana na miradi ya uchaguzi mkuu mwezi Septemba mwaka huu.

Naye Ndugu Hamisi Kasongo alitanabaisha kuwa kulikuwa na nafasi kubwa kwa mashirika ya dini kujihusisha na utoaji wa mafunzo ya elimu ya uraia.

Alisema hakukuwa na haja ya mashirika ya dini kungojea misaada kutoka nje kwa ajili ya kazi hiyo.

Hakuna sababu kabisa ya kuchelewa kiasi cha kukurupushwa na uchaguzi mkuu, alisisitiza.

Ndugu Kassongo alisema IRCPT ilikuwa na fursa kubwa, kwanza ya kuandaa mfumo mzima wa mafunzo ya elimu ya uraia na baadaye kutayarisha utekelezaji wa mafunzo endelevu ya elimu ya uraia.

Naye Ndugu Kassala alilitetea shirika la UNDP kwa kusema kuwa lilikuwa linaisaidia tu Tanzania katika jitihada zake za kujiletea maendeleo.

Lakini alisisitiza kuwa taasisi hiyo ya kimataifa haikuwa na wajibu wowote kwa serikali au kwa wananchi wa Tanzania.

"Wajibu wa kutoa elimu ya uraia kwa Watanzania ni ya Watanzania wenyewe, sio jukumu la UNDP," alisisitiza.

Ndugu Kassala alisema wajibu wa kwanza wa kutoa elimu ya uraia kwa Watanzania ni wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

"Tatizo langu ni kwamba tusije tukajifikisha mahali ambapo tutaendelea kutegemea misaada kutoka nje katika suala la kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wetu…kama nilivyokwishasema hili ni jukumu letu," alisema huku akionyesha wazi kwamba suala hilo hakuwa analichukulia mzaha.

"Hata hivyo alisema suala kubwa ni je, ni vipi suala zima la elimu ya uraia linaweza kufanywa endelevu?" aliuliza.

Akajijibu swali lake mwenyewe alisema; "nategemea viongozi wa dini watakuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Tukae pamoja ili tuweze kushughulikia suala hili," Ndugu Kassala alisema.

## 3. MAJIBU YA NDUGU MSHANA

Akijibu baadhi ya maswali, Ndugu Mshana alisema anavyojua yeye, hakukuwa na tatizo katika kupata mafunzo kwa ajili ya walimu wa kufundisha elimu ya uraia au mafunzo mengine yoyote yale.

Aliwaasa wote waliokuwa wanahitaji mafunzo kuendelea kushirikiana kati yao na nje ya mtandao wao.

Muhadhiri huyo hata hivyo hakuingia kwa undani juu ya kujiingiza kwa Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Jenerali Shimbo, lakini alisema sheria ilikuwa wazi kabisa katika suala hilo, alisema sheria hiyo ilikuwa inasema kazi ya kulinda usalama wa ndani na raia ilikuwa kazi ya Jeshi la Polisi. Kazi ya jeshi la ulinzi, JWTZ, ilikuwa kulinda mipaka ya nchi.

Baada ya kusema hivyo, Ndugu Mshana alimuomba Ndugu Kassala kumsaidia katika kujibu swali la tofauti kati ya kufuatilia (monitoring) na kuangalia (observe) uchaguzi.

Ndugu Kassala alisema kufuatilia uchaguzi (Monitoring) ilikuwa ni kuuangalia mwenendo wa uchaguzi na mwisho kutoa taarifa juu ya uchaguzi.

Lakini kuangalia uchaguzi(Observers) kulikuwa kunahusisha matumizi ya vigezo maalumu, katika zoezi hilo, kilichokuwa kinafanyika na waangaliaji au watazamaji wa uchaguzi ni kwa namna gani vigezo vilivyowekwa vilikuwa vimefikiwa na uchaguzi huo.

Alisema baadhi ya vigezo ambavyo vilikuwa vinaangaliwa ni kama vile suala zima la uchaguzi huru na haki, matokeo ya uchaguzi huo yana madhara gani kwa jamii na kadhalika.

***Suala la Zanzibar:***
Akijibu swali la faida inayoweza kupatikana katika serikali ya mseto, Ndugu Mshana alisema lilikuwa suala lisilopingika kuwa Zanzibar imekuwa ikikabiliwa na matatizo mengi kila uchaguzi mkuu unapofanyika.

Suala la uchaguzi visiwani Zanzibar limekuwa baya kiasi kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakidai kuwa uchaguzi mkuu haujawahi kufanyika katika visiwa hivyo!

Wengine wamekuwa wakisema kuwa kwa zaidi ya chaguzi mbili, chama tawala cha CCM, kilishindwa dhidi ya wahasimu wake, Chama cha Wananchi, CUF.

Ndugu Mshana alisema isitoshe kuna wakati watu kadhaa waliuawa kisiwani Pemba katika vurugu zilizokuwa zinahusiana na uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 (tukio hilo lilitokea mwezi Januari mwaka 2001 na inasadikiwa kuwa watu 23 waliuawa).

Itakumbukwa pia kuwa watu wengi walikimbilia nchini Kenya kutafuta hifadhi ya ukimbizi, tukio hili likiwa la kwanza katika historia ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, nchi ambayo kwa muda mrefu imekuwa kimbilio la wakimbizi kutoka kwenye nchi za maziwa makuu.

Ndugu Mshana alisema kuwa ikiwa kwa kufikia muafaka juu ya kuundwa kwa serikali ya mseto au umoja wa kitaifa, Wazanzibari watakuwa na uchaguzi mzuri, hilo litakuwa moja ya matunda ya serikali ya mseto.

Hata hivyo alisema kuwa pamoja na kufikiwa kwa muafaka huo kati ya viongozi wa pande mbili visiwani Zanzibar, suluhisho la kudumu katika matatizo mengi yanayoikabili Jamhuri ya Muungano na Zanzibar ni kuandaliwa kwa katiba mpya kabisa.

Ndugu Mshana alisema ukiangalia matatizo yote yaliyoelezwa na viongozi wa dini, kinachojitokeza ni kwamba matatizo karibu yote yanahusiana kwa namna moja au nyingine na suala zima la uteuzi wa viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Alisema kuendelea kuwepo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika mfumo na uteuzi wa viongozi wake, kunapunguza kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki.

Ndugu Mshana alisema kama taifa litaamua kutengeneza katiba mpya, basi suala la nafasi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi litapaswa kupewa kipaumbele ndani ya katiba hiyo.

Kuhusu suala la kuzuia kupeleka mahakamani matokeo ya kura za Rais, Ndugu Mshana alisema kuwa anafikiria uamuzi huo ulifikiwa ili kulinda hadhi ya kiti hicho. “Nadhani hatua hiyo ilifikiwa kuondoa uwezekano wa kutokea ombwe la uongozi katika nafasi hiyo,” alisema.

Hata hivyo baadhi ya washiriki wa dini mbalimbali ndani ya mkutano huo walisema kuwa hilo halikuwa hoja.

Walisema mtu mwingine angeweza kutafutwa kushikilia nafasi hiyo kwa muda mfupi wakati mchakato wa kumtafuta rais unaendelea.

Washiriki walisema pia kuwa kulikuwa na haja ya kuwepo na muda wa kutosha kabla ya kuapishwa kwa rais ili muda huo utumike katika kupokea malalamiko.

Walitoa mfano wa Marekani ambako rais mpya huapishwa baada ya kipindi cha miezi miwili.

Ndugu Mshana alipinga dhana ya kuwa Watanzania walikuwa wanapiga kura lakini walikuwa hawachagui viongozi wao.

Ndugu Riziki alizungumza kwa uchungu mkubwa juu ya tabia ya udanganyifu ambayo alidai inafanywa na chama tawala.

Alisema chama hicho kilikuwa na tabia mbaya ya serikali yake kutoa huduma muhimu kama vile maji wakati uchaguzi mkuu unakaribia.

Ndugu Riziki alitoa mfano wa eneo la Vingunguti, mjini Dar es Salaam hivi sasa wakazi wa eneo hilo wanapata maji baada ya kukosa huduma hiyo kwa zaidi ya miaka minne.

Ndugu Riziki alisema tukio hilo sio la kwanza, kiasi majuma machache kabla ya uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2005, wakazi wa eneo hilo walipata maji majuma machache kabla ya uchaguzi mkuu na mara baada ya hapo wahusika walichukua maji yao.

Ndugu Kassala alikuwa na maoni tofauti. Alisema hakukuwa na faida yoyote ya kulalamika, alisema kilichokuwa kinatakiwa kufanywa ni kuchukua hatua.

Naye Ndugu Bomani alisema wakati ulikuwa umefika kwa huduma muhimu kama vile nyumba, maji na elimu kuwekwa ndani ya katiba kama zinavyofanya nchi zingine barani Afrika kama vile Afrika Kusini.

Alisema hiyo ndio njia ya pekee ya kuhakikisha kuwa serikali ya Tanzania itatimiza wajibu wake.

Ndugu Bomani alisema Tanzania ilikuwa na utajiri mkubwa wa mali ya asili kama vile madini ambayo alisema yangeweza kutumiwa katika kuboresha uchumi wa nchi na hivyo kutatua, kwa kiasi kikubwa umaskini uliokithiri.



Alisema kinyume cha madai ya viongozi nchini, Tanzania si nchi maskini.

Tatizo kubwa la umaskini wa Tanzania, alisema, lilikuwa linatokana na utawala mbovu uliokuwa unasimamiwa kwa miongo kadhaa na viongozi wasiokuwa na dira na uadilifu.

Hata hivyo, Ndugu Mshana alisema kuweka mahitaji muhimu ya wananchi kama vile maji ndani ya katiba kunaifunga serikali kisheria kwa maana ya kuwa sasa inapaswa kutekeleza mahitaji hayo ama sivyo wananchi wanaweza kuishitaki serikali hiyo mahakamani.

Alisema kuwa nchi yoyote ile duniani haiwezi kuweka mahitaji hayo muhumi ndani ya katiba kama haina fedha za kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji hayo.

Mwezeshaji wa mkutano huo, Ndugu Salim Zagar alitoa mfano wa Misri ambayo alisema ilikuwa imeweka ndani ya katiba yake wajibu wake wa kumpatia kila mmoja wa raia wake mkate mmoja kila siku.

Alisema na hivi karibuni, Misri ilikabiliwa na tatizo kubwa la wapika mikate kutaka kuongeza bei ya bidhaa hiyo mara dufu, jeshi la nchi hiyo likachukua

jukumu la kuviendesha viwanda vya uzalishaji wa mikate kwa muda wa miezi mitatu wakati serikali ya nchi hiyo inatafuta namna ya kutatua tatizo la uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu. Ndugu Zagar alisema serikali ilichukua hatua hiyo kwa kuwa haingeweza kudiriki kushindwa kutatua tatizo hilo wakati ilikuwa imeahidi, kupitia katiba ya nchi hiyo, kuwa itampatia kila mmoja wa raia wake mkate mmoja kwa siku.

Naye Ndugu Kassala alisema wakati ulikuwa umefika kwa taasisi zinazosimamia imani, kuchukua hatua ili kuzuia nchi kuingia katika mivutano isiyo ya lazima kutokana na kuwanyima wananchi haki zao.

Alisema kuwa historia ilikuwa inaonesha kuwa kila wakati jamii ilikuwa inakabiliwa na matatizo kama vile wananchi kunyimwa haki zao, ndipo mitume na manabii walikuwa wakijitokeza kutoa uongozi wa kiroho kwa wananchi.

Ndugu Kassala alisema kama viongozi waliochaguliwa wanashindwa kutatua matatizo ya kijamii na kiuchumi nchini, basi viongozi hao hawafai.

Alisema anapinga madai ya baadhi ya viongozi kuwa serikali ya Tanzania ilikuwa maskini na hivyo isingeweza kutoa bure huduma muhimu kwa wananchi wake kama vile nyumba, maji na elimu Akijitolea mfano kuwa yeye binafsi alisoma bure kutoka shule ya msingi mpaka chuo kikuu, isitoshe, alisema, wakati huo pia walipatiwa maji safi.

Alisema hali hiyo ilitokana na kuwa na viongozi makini na waadilifu.

Alisema ukosefu wa ubinafsi uliwafanya viongozi hao kutumia vizuri raslimali chache za nchi zilizokuwepo katika kuboresha huduma za jamii kama vile elimu na afya.

Inamshangaza kuona hali hiyo imebadilika sana hivi karibuni pamoja na ukweli kwamba nchi ina raslimali nyingi zaidi sasa kuliko iliyokuwa wakati wa zamani.

Alisema matatizo mengi yanayoikabili nchi wakati huu yalikuwa yanatokana na mambo mengi vikiwemo kile alichokiita kuwepo kwa sera za uchumi na siasa huria.

Alisema la kusikitisha kuliko vyote ilikuwa kufikia hali ambayo wagombea wote wa kiti cha urais kutoka vyama vyote nchini kutozungumzia, katika hotuba zao za kampeni, mustakabali wa sera ya nchi ya visheni ya mwaka 2025 hadi leo.

Alisema kama viongozi wa nchi hawawezi hata kuzungumzia hilo, wanataka kuipeleka nchi wapi?

Je hao wana nia ya kuiendesha nchi bila dira?, aliuliza.

Alisema viongozi wa dini chini ya IRCPT, wanapaswa kuliangalia tatizo hili kwa undani kwa nia ya kupata ufumbuzi wa kudumu dhidi ya matatizo yanayoikabili nchi yetu kwa hivi sasa.

Ndugu Abdallah Tego kwa upande wake alivishambulia vyombo vya habari nchini kwa kuwa na tabia ya kutoa taswira ambazo si sahihi.

Alisema hivi karibuni alikuwa nchini Sudan ambako kwa mshangao mkubwa aligundua kuwa Rais Ndugu Omar al-Bashir ambaye hivi sasa anakabiliwa na mashtaka yaliyokuwa yanamtaka kupelekwa mjini Hague, nchini Uholanzi kwa makosa anayodaiwa kuyafanya Dafur, kusini magharibi mwa Sudan, kuwa ni kiongozi anayependwa sana ndani ya Sudan.

Alisema mtazamo huo ulikuwa kinyume kabisa na jinsi vyombo vya habari vya kimataifa na hapa nchini petu vimekuwa vikimwandika kiongozi hiyo.

Kiongozi huyo wa Sudan alisema amejijengea umaarufu huo kutokana na kwamba ni kiongozi pekee aliyewapa maendeleo makubwa kuliko viongozi wote waliyowahi kuitawala Sudan

Pili, alisema aligundua kuwa kinyume kabisa na jinsi vyombo vya habari vya kimataifa vimekuwa vikidai, tatizo la nchi hiyo ya Sudan lililopelekea vita vya wenyewe kwa wenyewe vya muda mrefu kuliko nchi yoyote barani Afrika, haikuwa inatokana na dini bali ubaguzi wa rangi.

“Ndio sababu hivi sasa dunia imeshikwa na butwaa kuhusu matatizo ya Dafur kwani asilimia kubwa ya wakazi wa jimbo hilo ambao ni weusi ni waislamu kinyime cha wale wa Sudan ya kusini ambao asilimia kubwa ni wakristo,” alisema.

Ndugu Tego alisema kuwa kutokana na propaganda hizo za vyombo vya habari vya nje na hapa nchini, alikuwa amejiamulia kutosoma kabisa magazeti ya hapa nchini.

Ndugu Kasongo kwa masikitiko makubwa alisimulia juu ya jinsi mama mjamzito alivyopoteza kichanga chake kutokana na matatizo ya usafiri huko Kibaigwa, katika wilaya ya Kongwa wakati wananchi walijitahidi kumuwaisha mama

huyo hospitalini kwa kutumia mkokoteni, lakini walikuwa tayari wamekwisha chelewa!


Ndugu Kasongo alisema tukio hili lilikuwa la aibu sana hasa ikizingatiwa kuwa matukio ya aina hii yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika nchi ambayo ipo uhuru kwa karibu miongo mitano sasa.

Karibu washiriki wote walikuwa wanakubaliana juu ya haja ya kutayarisha mfumo mmoja wa ufundishaji wa elimu ya uraia na kuanza kazi ya kutoa elimu hiyo kwa wananchi kila wakati badala ya kungojea mpaka karibu na kipindi cha uchaguzi mkuu.

Washiriki hao kwa pamoja walikubaliana kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa vizuri chini ya IRCPT.

Ndugu Erasto Ndeuka mmoja wa maafisa kutoka KAS aliwauliza washiriki hao ni kwa kiasa gani washiriki wanahusika, kwa namna moja au nyingine, katika matatizo ambayo yanaikabili nchi kwa hivi sasa?.

“Ni kwa kiasi gani mashirika yetu ya dini (FBO) yalikuwa yanahusika katika kutatua matatizo yanayoikabili nchi yetu hivi sasa?, aliuliza.




Ndugu Ndeuka, akayataka masharika ya dini kuwaelimisha wananchi, kuanzia elimu ya uraia, kwa nia ya kuwaweka katika nafasi ya kujikwamua kutokana na matatizo ambayo yanawakabili.

Aliwataka pia kuanza kuangalia uwezekano wa kuwahamasisha wananchi juu ya haja ya kuishinikiza serikali kuandaa kwa ushirikiano nao katiba mpya ya nchi.

Wito wa afisa huyo wa KAS ulitokana na mtazamo uliotolewa mapema na washiriki hao kwa kuwataka wananchi washinikize serikali kutayarisha katiba mpya wakati wengi wa wananchi hawajui hata rangi ya katiba licha ya yaliyomo ndani ya katiba ya hivi sasa.

Washiriki walisisitiza haja ya mashirika ya dini kwanza kuwaelimisha wananchi, kupitia elimu ya uraia, juu ya yale yaliyomo ndani ya katiba ya hivi sasa kabla ya kuzungumzia umuhimu wa kuwa na katiba mpya.

Ndugu Ndeuka alisema mara tu wananchi walio wengi, hususani waishio vijijini, watakapopewa elimu ya uraia na yale yaliyomo katika katiba yao ya hivi sasa itakuwa rahisi kushughulikia katiba mpya kwa wepesi, kwani raia wengi watakuwa wanajua wajibu na wafanye mabadiliko yapi, wapi na kwanini kama walivyofanya wenzao nchini Kenya.

Afisa huyo alisema kulikuwa na haja kubwa kwa IRCPT kujihusisha kwa makusudi katika mipango ya ushiriki wao kama wafuatiliaji na waangalizi wa uchaguzi mkuu, kuanzia uchaguzi ujao.

Alisema IRCPT, wanapaswa kuangalia ushiriki wao kama wafutiliaji na waangalizi wa chaguzi nchini katika mpango wao wa muda mrefu ambao utaangalia, kwa mfano, kipindi cha umbali wa miaka ishirini ijayo.

“Uzuri wa ushiriki wenu kama wana dini ni kwamba mnawajua ni kina nani katika waumini wenu wanajihusisha na rushwa na ufisadi.

Alimalizia kwa kusema kuwa viongozi wa dini kupitia IRCPT, watapata wepesi kuleta mabadiliko ya haraka na tija katika mfumo mzima wa uchaguzi hapa nchini.”

Ndugu Mwinyimvua aliwalaumu viongozi wa dini kwa kushindwa kushiriki, kikamilifu, katika masuala husika

Alisema hayo wakati alipokuwa akijibu malalamiko kutoka kwa mshiriki kuwa shirika lake la dini lilikuwa kila mara linaachwa, kila inapotokea nafasi ya kupata mafunzo yaliyokuwa yanatolewa na wafadhili kutoka nje ya nchi na mambo mengine muhimu ya maendeleo.

Ndugu Mwinyimvua aliwataka viongozi wote wa dini ndani ya IRCPT kutumia mitandao yao ndani na nje ya jukwaa hilo kuwasiliana na wenzao na wafadhili kutoka nje, hatua ambayo alisema itawasaidia kupata misaada mbalimbali badala ya kulalamika.

Alisema ni kwa ushirikiano wa karibu kati na baina yao ndio tu wanaweza kufanikiwa chini ya jukwaa lao la dini katika kuhakikisha kuwa serikali inatekeleza yale tu yaliyokuwa na tija kwa nchi kuanzia kwenye zoezi zima la uchaguzi mkuu.

Malalamiko juu ya kunyimwa misaada, upendeleo uliodaiwa kufanywa na wafadhili wa nje kwa baadhi ya mashirika ya dini, utoaji wa tenda kwa vigezo vya kujuana na sio kwa uwezo yalitawala mazungumzo katika mkutano huo.

Hata hivyo mmoja wa washiriki katika mkutano huo alisema malalamiko hayo hayakuwa mageni.

Alisema malalamiko ya aina hiyo pia yalitolewa katika mkutano uliofanyika mwezi Septemba, mwaka 2009 mjini Tanga.

Mshiriki huyo alisema mchakato wa tenda siku hizi ulikuwa wa wazi sana.

Alisema kinyume cha madai ya kuwepo kwa uonevu na upendeleo, ukweli wa mambo ulikuwa, wale walioshindwa kupata tenda hizo walishindwa chini ya misingi ya kiufundi.

Aliwataka wale ambao wamekuwa wakishindwa badala ya kulalamika kuwatumia wenzao ndani ya IRCPT ambao wana uweledi mkubwa na uzoefu katika mchakato mzima wa zabuni.

Naye Mchungaji Mallya aliishutumu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa madai kuwa ilikuwa ikipendelea baadhi ya mashirika ya dini ambayo katika utoaji huduma.

Mchungaji Mallya alitaka IRCPT kulalamika kwa maandishi kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi juu ya suala hilo.

Kwa mara nyingine tena, Mchungaji Mallya alilalamika kuwa yaliyomo katika kijitabu kilichochapishwa na wafadhili wa mkutano huo, KAS, kilichopewa kichwa cha Wajibu wa Mashirika ya Dini katika Utawala Bora yalikuwa hayawakilishi yale yaliyozungumzwa katika mkutano wa mashirika ya dini.

Alidai kuwa Ukristo ulikuwa umekandamizwa ndani ya kijitabu hicho kwa kupendelea Uislamu.

Ndugu Kassala alimtaka Mchungaji huyo kuthibitisha ni yepi yaliyokuwa yamechapishwa katika kijitabu hicho hayakuwa yamezungumzwa katika mkutano husika.

Washiriki wawili, waliochangia ndani ya mkutano huo, walithibitisha kuwa yote yaliyokuwa yamechapishwa ndani ya kijitabu hicho yalizungumzwa kwenye mkutano kusika na kuwa ni sahihi.

## MAONI/MAPENDEKEZO YA WAWAKILISHI WA VIONGOZI WA MASHIRIKA YA KIDINI NCHINI TANZANIA

Maoni yaliyotolewa, kwa maandishi, na wawakilishi wa viongozi wa dini kwenye mkutano wa siku tatu uliofanyika katika Hoteli ya Land Mark, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam. Maoni haya yalikuwa yakitolewa kila mkutano huo unapokaribia kufungwa jioni. Maoni haya ni majumuisho ya maoni yaliyoanza kutolewa kutoka tarehe 11 jioni mwezi Oktoba, tarehe 12 na mwisho wa mkutano huo, tarehe 13.

**Changamoto kwa Mashika ya Dini**

1. Kwa kuwa Taasisi za Dini zinapata msamaha wa kodi kwa vifaa vinavyotumika kwa ajili ya masuala ya jamii (afya, shule, n.k). FBOs washauriwe kupunguza gharama za huduma zao kwa wananchi.

2. FBOs wabadilike ili waweze kufanya kazi kwa hekima, umoja na amani kwani wanapaswa kufahamu kuwa sauti ya wengi ni sauti ya umma na husikika mbali.

**Ushauri kwa Serikali:**

(a) FBOs washirikishwe katika kuandaa mutaala kwa ajili ya elimu ya uraia nchini kote.

(b) FBOs washirikishwe katika kubainisha sifa za kiongozi bora, na ili liwekwe kwenye mtaala.

(c) Baada ya nambari 1 na 2 kufanyiwa kazi, serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha uchaguzi bila kampeni. Kwa mfano, kwa kuwa uchaguzi unaanzia kwenye ngazi ya kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa, na mwisho taifa. Ni wazi kuwa kote huko wapigiwa kura watakuwa wanajulikana kwa wapiga kura, kitabia. kimaadili, n.k

**Michango Zaidi ya Wawakilishi:**

(1) Kuna nyaraka zilizotolewa na Taasisi mbalimbali za kidini kuhusiana na uchaguzi. Nyaraka hizo zipitiwe na IRCPT na pale watakapopata maoni na mapendekezo yanayofaa, basi yaingizwe kama sehemu ya mchango wa wananchi katika elimu ya uraia na uchaguzi.

(2) Jumuiya za kidini zipewe nafasi ya pamoja ya kueleza sifa za kiongozi bora na njia za kuwapata viongozi hao.

(3) Kwa mfano, mtuhumiwa wa rushwa asiruhusiwe kushiriki kama mgombea wa nafasi ya uongozi hadi hapo kesi yake itakapokwisha.

(4) Rais atoe maelezo ya mali zake baada ya kuisha kipindi chake cha uongozi; na watu waruhusiwe kumhoji juu ya uhalali wa mali alizonazo.

(5) Viongozi nchini hawana upendo na uzalendo kwa nchi yetu na wananchi wake kwa ujumla. Hii inatokana na kushindwa kwa viongozi hawa katika kutoa huduma za msingi za kiuchumi na kijamii za kuinua uchumi wa mtu mdogo na taifa ili lisiwe tegemezi, kutowafikia wananchi walio wengi. Huduma za umeme, maji na miundombinu hazijawafikia wananchi wengi, hasa waliofukara.

**Katiba Iangalie Haki za Wazee na Watoto:**

1. Wazee wamesahaulika sana katika katiba ya nchi yetu. Kila mtu akijaliwa, hatimaye atakuwa mzee. Sasa unapofikia hali hiyo inakuwaje kama sasa hutufanyi maandalizi ya aina yoyote kwa ajili ya wazee wetu waliopo hivi sasa? Uzoefu unaonyesha kuwa mbali na kushughulikia matatizo yao ya uzee, wazee walio wengi ndio walezi wa watoto ambao wazazi wao wamefariki kwa maradhi mbali mbali, hususani ugonjwa wa Ukimwi. Sasa sisi kama wawakilishi wa FBOs, tunaieleza nini serikali yetu kuhusu wazee hawa?

    - Je serikali yetu inawachukuliaje wazee wa mitaani? Ikiwezekana, suala hili litafutiwe ufumbuzi wa kudumu ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hili katika jamii yetu.

**Suala la Watoto wa Mitaani:**

1. Hatujapata nafasi ya kujua kwa undani nafasi ya mwanamke katika Katiba ya nchi katika ngazi za maamuzi. Hivyo kamati teule iangalie na kuboresha hali hii.

**Kuhusu: Katiba**

1. Kwenye katiba ya IRCPT, ambayo bado inaendelea kuboreshwa, makundi maalumu kama vile ya wanawake na watoto, yamepewa nafasi ya kuwakilishwa katika ngazi ya governing board (ambayo hujihusisha na maamuzi).

2. Tunapendekeza pia kuwepo kwa tume ya Ukweli, Maridhiano na Amani ili iweze kutusaidia pale zitakapojitokeza dalili za kutofautiana.

## KUFUNGA

### MTAZAMO WA KAS KATIKA MIKUTANO YA USONI YA IRCPT:

Akizungumza kwa niaba ya wafadhili wa mkutano waWawakilishi wa Vingozi wa Mashirika ya Dini yanayoshughulikia Amani nchini Tanzania, IRCPT, taasisi ya Ujerumani ya Konrad Adenauer Stiftung, KAS, Kiongozi wa Timu, Ndugu Richard Shaba, aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria mkutano huo.

Alisema kwa maoni yake, mkutano huo ulikuwa umefanikiwa katika kufikia malengo ambayo yalikuwa yamepangwa na mkutano huo.

Alisema kuwa ijapokuwa alikuwa hapendelei kutoa ahadi, hata hivyo taasisi hiyo ya Kijerumani yenye ofisi yake mjini Dar es Salaam ingeangalia uwezekano wa kuwa na mikutao mingi ya aina hiyo.

### JE IRCPT NI NINI?

Kabla ya kufungwa kwa pazia la mkutano, Muwezeshaji, Ndugu Salim Zagar, alimkaribisha Katibu Mkuu wa IRCPT, Ndugu Ayoob Omari kuwaeleza wajumbe waliohudhuria mkutano huo kazi ya jukwaa hilo la IRCPT.

Kutoka mwanzo kabisa, Ndugu Omari alisema hangezungumzia kirefu juu ya IRCPT, kwa kuwa jukwaa hilo tayari lilikuwa na chapisho ambalo lilikuwa limeeleza wasifu wa jukwaa hilo kwa undani na kwa kirefu.

Kitu kingine ambacho hakukizungumzia, ijapokuwa kilikuwa kinasaidia madai yake, ni kwamba idadi kubwa ya wajumbe katika mkutano ule walikuwa wanawakilishi viongozi wa mashirika ya dini katika jukwaa hilo.

Kwa hiyo haiingii akilini kuwa wajumbe hao wanaweza kuwakilisha viongozi wa dini kutoka jukwaa hilo na halafu wasijue wasifu wa jukwaa hilo.

Kutokana na hilo, Ndugu Omari alitumia nafasi aliyopewa na Ndugu Zagar, kujibu, kwa ujanja na umahili mkubwa, baadhi ya maswali au maoni yaliyokuwa yametolewa wakati wa mkutano huo, maswali na maoni ambayo yalikuwa yameibua masuala tete, mengine yakiwa na mtazamo wa kidini.

Moja ya masuala hayo tete yalihusiana na ushiriki wa Wakristu na Waislamu katika serikali za Tanzania tokea kupatikana kwa uhuru na Muungano kati ya serikali za

Tanganyika na Zanziar, kufuatia Mapinduzi ya Visiwa vya Zanzibar.

Ndugu Omari alisema uchache wa wafanyakazi/maafisa Waislamu katika serikali za mwanzo za Tanganyika, na baadaye Tanzania, kwa kiasi kikubwa, lilikuwa suala la kihistoria.

Kwa mfano alisema shule nyingi hapa nchini, hususani Tanzania Bara, zilikuwa zimeanzishwa na kumilikiwa na madhehebu ya kikristu.

Kadri miaka ilivyokuwa ikipita, idadi ya wasomi wakristu iliendelea kuongezeka mara dufu huku ile ya Waislamu ikiendelea kuwa chini.

Itakumbukwa kuwa ni kutokana na hali hiyo, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipoamua kutaifisha baadhi ya shule hizo za madhehebu ya kikristu, nia yake ikiwa kuhakikisha kuwa Waislamu na watu wa madhehebu mengine na wale wa dini za kienyeji wanapata nafasi katika shule hizo, na hivyo kuondoa kuendelea kwa tofauti za elimu katika waumini wa dini mbalimbali hapa nchini.

Kwa kufanya hivyo, nia ya Mwalimu ilikuwa kujenga taifa moja na siyo nchi ya vipande vipande ambayo baadaye ingeibua mifarakano katika taifa.

Akitoa mfano wake mwenyewe, Ndugu Omari alisema alipoteuliwa na serikali kuwa mkuu wa shirika moja nchini, ndugu yake wa damu ambaye alikuwa Mkristo na ambaye walikuwa wamekua wakisoma na kutokea katika nyumba moja, alionekana kushangazwa sana na uteuzi huo wa serikali, hasa ikizingatiwa kuwa yeye alikuwa Mwislamu!

Anasema mshangao wa ndugu yake haukuwa unatokana na kwamba hakuwa anastahili kuteuliwa katika nafasi hiyo, la hasha.

Mshangao ule ulitokana na ukweli kuwa yeye hakuwa Mkristo na kwamba uteuzi wake katika nafasi hiyo ulikuwa moja ya teuzi chache sana zilizowahusisha Waislamu.

“Wakati mwingine mshangao huo hautokani na kwamba mtu anapinga uteuzi ule, la hasha ni mshangao tu unaotokana na kwamba si jambo la kawaida. Kwa mfano kwa yule ndugu yangu, alifurahi kuchaguliwa kwangu. Kwani mimi nilikuwa ndugu yake. Lakini hili halikumzuia yeye kushangaa,” alisema Ndugu Omari.

Waislamu hawakuwa wanateuliwa kwa sababu wengi wao hawakuwa na elimu ya juu, anasema Ndugu Omari.

"Kwa kifupi, uteuzi wa Waislamu wakati huo haukuwa jambo la kawaida, na siyo kwa sababu walikuwa hawapendwi, la hasha. Ukweli ni kwamba walikuwa wachache sana wakati huo waliokuwa wana elimu ya kutosha kushikilia nyadhifa kubwa za uongozi katika mashirika yaliyokuwa yanahitaji utaalamu mkubwa," anasema Ndugu Omari.

Katibu Mkuu huyo wa IRCPT alisisitiza umuhimu wa kuwa na uvumilivu katika masuala ya dini, kwamba watu, na hususani waumini wa dini mbalimbali hapa nchini, wanapaswa kuwa wavumilivu miongoni mwao na kati yao ndani ya dhehebu moja moja na kati yao na waumini wa dini nyingine.

Alisema hili linapaswa kuanza kusimamiwa kuannzia katika jukwaa la IRCPT.

Kwa kifupi, alisisitiza haja ya kulitumia jukwaa hilo kikamilifu katika kujenga, sio tu uvumilivu wa kidini, bali pia kutumia jukwaa hilo katika kutatua matatizo mbalimbali ambayo yatakayokuwa yakilikabili taifa.

Ndugu Omari alisema katika nchi moja ya Ulaya ambako aliwahi kuishi kama mwanafunzi, waumini wa dini moja walikuwa asilimia 80.

Alisema wananchi katika nchi hiyo walikuwa waadilifu sana katika masuala mbali mbali ya maisha ya kila siku, masuala ya utendaji wa kazi.

Lakini jambo la kushangaza ni kwamba ni wachache sana katika asilimia hiyo 80 walikuwa wanakwenda kwenye majumba ya ibada siku ya Jumapili.

Lakini ukitoa mlinganisho wa nchi ile na Tanzania utakuta jambo la kushangaza.

Idadi kubwa ya waumini wa dini mbalimbali hapa nchini (theluthi mbili kufuatana na Mhadhili wa Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndugu Ebenezer Mshana) wanakwenda kwenye majumba ya ibada Ijumaa, Jumamozi na Jumapili.

Lakini ukifanya ulinganishi kati ya nchi ile ya Ulaya na Tanzania, anasema utaona tofauti ya kutisha katika suala la zima la uadilifu, kwamba hapa nchini Tanzania uadilifu miongoni mwa wananchi ni tatizo kubwa!

Ndugu Omari alisema wakati ulikuwa umefika kwa wananchi wa Tanzania, na hususani wale waliokuwa wafuasi wa madhehebu na dini mbalimbali kunyanyua viwango vya uadilifu ili viende sambamba na mahudhurio yao katika majumba ya ibada, uaminifu na imani waliyonayo katika madhehebu na dini zao mbali mbali.

## SHUKRANI:

Ndugu Camillus Kassala alitoa shukrani, kwa niaba ya wawakilishi wa viongozi wa mashirika ya dini, IRCPT, kwa taasisi ya Ujerumani ya Konrad Adenauer Stiftung kwa kugharamia uandaaji wa mkutano huo wa siku tatu.

Katika hotuba yake fupi iliyokuwa imejaa filosofia, Ndugu Kassala, alizungumzia kwanini watu wengi walikuwa mara kwa mara wakikabiliwa na matatizo mbalimbali.

Alisema siyo kila wakati kitu ambacho machoni mwa mwanadamu kilikuwa kinaonekana halisia kilikuwa ni kitu kizuri.

Alisema kadhalika katika masuala yanayohusiana na maadili. Alisema sio kila kitu kinachoonekana kuwa kinaweza kutekelezwa vizuri kilikuwa kinakidhi mizani ya uadilifu.

Kwa kifupi, alisema utekelezaji wa kitu fulani unawezekana kuonekana ni sawa, lakini hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza kitu au hatua hiyo inaweza kuwa inakwenda kinyume cha maadili.

Mtu anaweza kutoa fedha, kama hongo, (mfano wa mwandishi) ili atibiwe na kweli mtu huyo akatibiwa na kupona. Lakini kimaadili, hatua aliyochukua mtu huyo ina mapungufu makubwa ya uadilifu.

Kwa hiyo, alisema Ndugu Kassala, ikiwa watu wanakupinga, inawezekana kabisa kuwa kitu unachotaka kutekeleza au unachokipenda kinagongana na uadilifu. Haya masuala yanapaswa siku zote kutazamwa kwa uangalifu, alisisitiza.

Ndugu Kassala aliwashukuru viongozi wa taasisi hiyo ya Ujerumani ya KAS kwa kugharamia mkutano huo na kusema kuwa mkutano huo ulikuwa umesaidia sana kuwaleta wawakilishi wa viongozi wa dini hapa nchini karibu zaidi.

Alisema ukaribu huo sasa utasaidia katika kujenga ushirikiano katika kutatua matatizo mbalimbali yanayolikabili taifa, kuanzia matatizo yenye mtazamo wa kidini mpaka matatizo ya kisiasa na kiuchumi.

# VIAMBATISHI

## Kiambatishi 1: MADA ZILIZOWASILISHWA

### 1. Mada ya Ndugu Bernard Okok-Obuoga kwenye mkutano wa Wawakilishi wa Viongozi wa Mashirika ya Dini (IRCPT) aliyoitoa kwenye Hoteli ya Land Mark, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam tarehe 11, Oktoba, 2010

Nina furaha kubwa ya kuwepo kwenye mkutano huu wa wawakilishi wa viongozi wa mashirika ya dini, mkutano ambao madhumuni yake ni kupanga mikakati ya kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu mwaka huu unakuwa huru na wa haki.

Napenda kutoa pongezi zangu kwenu kwa kujihusisha na juhudi hizi. Kadhalika, ningependa kuwafikishia salamu kutoka kwa Viongozi wa Mashirika ya Dini barani Afrika, viongozi wanaosimamia dini kwa ajili ya amani, (ACRL-RfP.

Napenda pia, kwa niaba yangu na ya wafanyakazi wenzangu, kutoa shukrani zetu za dhati kwa ofisi ya taasisi ya Konrad Adenauer (KAS-Tanzania), nchini Tanzania kwa imani waliyonayo kwa Viongozi wa Masharika ya Dini nchini Tanzania, IRCPT na kwa kutoa, pamoja na mambo mengine, msaada wa fedha kugharamia tukio hili na mengine kwa ajili ya jumuiya za dini.

Ni matumaini yangu kuwa tukio hili litafungua ukurasa mpya katika milango ya ushirikiano kwa kuchochea ushirikiano zaidi katika siku usoni.

Kwa wale wanaosikia kwa mara ya kwanza, shirika la Viongozi wa Mashrika ya Dini Barani Afrika-ACRL-RfP, kwa kifupi, hili ni jukwaa kubwa la dini kuliko yote barani Afrika.

Jukwa hili pia lina uwakilishi mkubwa wa madhehebu mbalimbali ya dini barani Afrika.

Lengo letu, pamoja na mambo mengine, ni kuhamasisha jamii za kidini na viongozi wake barani Afrika ili kwa pamoja waweze kuhakikisha uwepo wa amani, haki na maelewano kati na miongoni mwa jamii zao.

Ili kuweza kufanikiwa katika haya, tumejiwekea malengo yatakayotuwezesha kuondoa migogoro na kusimamia maendeleo endelevu; kusimamia uwepo wa amani kati na mingoni mwa jamii mbalimbali.

Kazi nyingine ni kujenga heshima na dhana ya utayari na kukubali dini za waumini wengine ndani na nje ya dini zao; kuendesha na kusimamia utatuzi wa migogoro ndani na nje ya jumuiya mbalimbali; kuendesha na kusimamia ushirikiano kati na baina ya Mashirika ya Kitaifa ya Viongozi wa Dini Barani Afrika (NIRCs), Mashirika ya Dini ya Kusini mwa Afrika (SIRCBs), Mashirika ya Imani ya Wanawake na Mtandao wa Vijana.

Nia ya kuviendesha na kuvisimamia vyombo hivi vilivyotajwa hapo juu ni kuhakikisha vinakuwa tayari katika kupambana na changamoto zinazojitokeza mara kwa mara.

ARCL-RfP kimekuwa chombo ambacho wakati wa hatari na machafuko katika nchi mbalimbali barani Afrika, kimekuwa kikijiweka katika mstari wa mbele katika utatuzi wa migogoro katika nchi hizo.

Kadhalika, chombo hiki kimekuwa kikitoa msukumo, kwa nchi za Afrika, katika uzingatiaji wa haki za binadamu, haki na utawala wa sheria.

Mpaka sasa ni siku chache sana zimebaki kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Kutokana na hali hiyo, kwa maoni yangu, kutokana na muda mdogo uliobakia, mna nafasi ndogo sana ya kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu unakuwa huru na wa haki.

Kwa hiyo, ningependa kuwashauri mtumie mkutano huu kuangalia chaguzi zijazo, kwani mnapaswa kuuangalia uchaguzi mkuu sio tu kama tukio, bali kama mchakato mzima.

Kwa kifupi, mnapaswa kuangalia uchaguzi mkuu kutoka kwa wapigaji kura mpaka zoezi zima la uandikishaji wa wapiga kura hao, kutoka vyama vya siasa mpaka kampeni za vyama hivyo na kutoka ilani zao za uchaguzi mpaka sera zao.

Kwa hivyo mashirika ya dini yanapaswa kuangalia mchakato mzima wa uchaguzi, siyo sehemu tu ya uchaguzi huo.

Katika kuangalia suala zima la uchaguzi na nafasi ya mashirika ya dini, nimeona mmeweka mkazo katika suala la elimu ya uraia na nafasi ya mashirika ya dini kupitia muungano wao wa FBO.

Katika shirika la viongozi wa dini barani Afrika, msisitizo ukiwa dini kwa ajili ya amani, ARCL-RfP, tumekuwa tukishikilia kuwepo kwa msimamo wa pamoja katika kuhamasisha viongozi wa dini na jumuiya zao katika kusimamia ujenzi wa amani, haki na ushirikiano katika jamii zao.

Moja ya vitu muhimu katika hili ni uandaaji, kwa pamoja, wa ajenda moja kwa jamii ambayo inachochea uwepo wa chaguzi huru na za haki. Ni kutokana na hili, mkutano wenu wa siku tatu una mchango mkubwa sana.

Katika mada yangu juu ya nafasi ya masharika ya dini katika kuchochea uchaguzi huru na wa haki, pamoja na kugusia uzoefu wa Kenya katika suala hili; nitaangalia mategemeo ya watu kwa mashirika ya dini katika suala hili tunalolizungumzia.

Na baada ya hapo, nitachambua hali iliyopo hivi sasa. Kadhalika, katika mada hii, tutaweza kuona mapengo yaliyojitokeza na namna mapengo hayo yalivyosaidia, baadaye katika kuleta machafuko nchini Kenya baada ya uchaguzi ule.

Napenda kuamini kuwa watu wamejifunza mengi kutokana na yale yaliyotokea nchini Kenya.

Viongozi wa mashirika ya dini nchini Tanzania, IRCPT, chama chao kikiwa moja ya vyama 23 vya aina hiyo barani Afrika ambavyo viko chini ya ACRL-RfP, kinatakiwa kuzingatia yaliyotokea nchini Kenya kama changamoto kwa kuchukua hatua zinazopaswa.

Hatua hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwa viongozi wa dini, jumuiya na mashirika yao yanachukua hatua ya pamoja katika kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu unakuwa huru na wa haki.

## 2. <u>Imani za dini na mashirika ya dini katika jamii</u>

Naomba mniruhusu kuchanganya matumizi ya imani za kidini (faiths) na dini (religions) katika mada yangu, pamoja na kuwepo kwa tofauti ndogo katika maneno hayo mawili.

Ningependa kuanza kwa kusema kuwa dini ni dhamira ya jamii, hivyo kuna haja kubwa ya kuhakikisha kuwa misingi ya ubinadamu (maadili) inasimamiwa katika jamii.

Kutokana na hili, dini au mashirika ya dini yanapaswa kutumiwa kama chombo cha kuhakikisha kuwa misingi hii ya jamii sio tu inapatikana, bali pia inaendelezwa katika jamii.

Ningependa pia kuisisitiza kuwa pamoja na ukweli juu ya nafasi ya mashirika ya dini katika kusimamia misingi ya binadamu katika jamii, lakini hakuna shirika moja linaweza kufanya kazi hiyo peke yake, na hili siyo Tanzania tu, bali duniani kote.

Kwa maana hiyo, ni lazima kuwepo na ushirikiano kati ya, na baina ya mashirika ya dini ili kuweza kupambana na kushinda dhidi ya changamoto mbalimbali za kibinadamu hapa duniani.

Kutokana na hilo, kuundwa kwa mtandao wa mashirika ya dini kwa nia ya kupambana na changamoto mbalimbali zinazokabili jamii, ni mojawapo ya matatizo mengi ambayo yanayakabili mashirika ya dini.

Moja ya changamoto kubwa ni maana nzima ya mtandao unaoundwa na dini mbalimbali au kile kinachojulikana siku hizi kama mazungumzo ndani ya dini mbalimbali.

Ijapokuwa suala hili linahitaji kuangaliwa kwa kina siku nyingine, kwa leo ningependa kujikita katika masuala ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika mfumo mzima wa mtandao mmoja wa dini mbalimbali.

KUKUBALI: Waumini wa dini wanapaswa siku zote kukubali kuwa wataendelea kuwa tofauti na waumini wa dini nyingine.

Na ili kuendelea kubeba mzigo wa kuwa dhamira ya jamii, tunapaswa kuelewa, kukubali na kupenda tofauti zetu za kidini na kiutamaduni kwa kuzifanya tofauti hizo kuwa nguzo kuu za kufanya kazi pamoja.

Vitabu vyetu vitakatifu vyote vina mafundisho kadhaa yanayoonyesha umuhimu wa sisi kama binadamu kuishi katika udugu.

Kwa mfano, katika Uislamu, Quran inawataka Waislamu wote kama ifuatavyo:

*Ewe binadamu! Tumekuumba kutokana na roho moja, mwanaume na mwanamke, na tumekuumba wewe katika mataifa na makabila, ili muweze kufahamiana. Kwa hiyo anayeheshimiwa mbele ya Mungu ni yule anayemuabudu Mungu. Mungu ni muelewa, Mungu anajua yote (49:13).*

Msingi wa ujirani mwema unawataka waumini wa dini wote kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano na siyo kwa kuuana. Huu ni msingi mkubwa katika ushirikiano wa mashirika ya dini.

Ili kujenga msingi madhubuti katika jukwaa letu la mashirika ya dini, hususani katika suala zima la utawala bora katika jamii kuanzia katika kuhakikisha uwepo wa uchaguzi mkuu ulio huru na wa haki nchini, waumini wa dini wanapaswa kujenga dhana ya *kuaminiana* kati na baina yao.

Hili linawezekana tu ikiwa tutaelewa na kupendana katika tofauti zetu za maisha. Njia rahisi ya kufanikisha hili ni kwa kutekeleza kile kinachojulikana kama 'the Golden Rule' au mafunzo ya kidini.

| | |
|---|---|
| **Judaism:** | ***"Unachokichukia wewe; usimtendee mtu mwingine. Hii ni sheria. Mengine ni tahariri tu." Talmud, Shabbat 3 la.*** |
| **Islam:** | ***"Hakuna kati yenu (kwa kweli) anaamini mpaka anapotaka kaka yake afikiwe na mazuri aliyoyapata yeye." Number 13 of Imam "Al-Nawawi's Forty Hadiths"*** |
| **Baha'i Faith:** | ***"Usimuombee mtu usichotaka mwenyewe kuombewa. Usimseme mtu kitu ambacho mwenyewe hungependa kusemwa."*** <br><br> ***"Mbarikiwa ni yule anayetaka kaka yake afanikiwe badala yake." Baha'u'llah*** |
| **Christianity:** | ***"Kwa hiyo katika yote, watendee wengine yote ambayo ungependa kutendewa mwenyewe kwani hili ni jumuisho la Sheria na Mitume" Matthew 7:12 (NIV)*** |

Kupitia nukuu hizi kutoka vitabu vitakatifu, tunaweza kujenga mahusiano mazuri kati yetu na waumini wa dini nyingine mbalimbali, na hivyo kutumia nguvu zetu kwa pamoja katika kuimarisha umoja wetu utakaotokana na utatuzi wa pamoja wa matatizo yetu.

Katika ARCL-RfP, tunachochea, pamoja na mambo mengine misingi, ya *uelewa* na *kuheshimu* tofauti za dini zetu na maamuzi yetu yanasimamiwa na maadili yanayokubalika kote.

Nchini Tanzania, kwa pamoja mumeamua kuwa suala la uchaguzi mkuu ulio huru na wa haki ni jambo muhimu kwenu, na mumeamua kukutana kwa ajili ya kupanga mkakati wa kulishugulikia suala hili kwa pamoja.

Jumuiya za kidini, hususani, mashirika ya dini yanapaswa *kujenga utamaduni sio tu wa kuishi pamoja, bali pia kupiganiana*.

Lengo hili linaweza kufikiwa kwa kusimamia vitu vikubwa viwili; ukweli na kulindana, hata kama dini zenu ni tofauti.

Katika Uislamu, dhana ya *Dhimni* inakuja akilini; na katika Ukristu, dhana ya ile hadithi ya mwanamke aliyedaiwa kukutwa, na kundi la wanaume katika tendo, kufikishwa kwa Yesu Kristu inahusika.

Hii ni changamoto kwako na mimi kuwalinda wanyonge katika jamii. Kwa mfano, nina uhakika kuwa kama Waislamu nchini Tanzania watawatetea waumini wa Baha'i katika lolote lile baya dhidi yao, wafuasi wa Baha'i watawaamini na kuwaona Waislamu kuwa ni ndugu zao.

Kwa hiyo ni muhimu kwa mashirika ya dini kuzingatia dhana hii muhimu.

*Dira na uongozi* wa mashirika ya dini unapaswa kusimamiwa na viongozi wa dini.

Kwa hiyo, majukwaa yanayowaleta pamoja viongozi wa dini na jumuiya zao, kama vile IRCPT, yanatakiwa kuhakikisha kuwa viongozi hao wa dini wanasimamia kikamilifu dira zao.

Hii ina maana ya kuwa taasisi hizo zinapaswa ziongozwe, zimilikiwe na kuendeshwa na viongozi wa dini katika nchi husika.

Katika ACRL-RfP, dira na malengo ya chama yanasimamiwa na viongozi wa juu ambao wanasimamia uhamasishaji wa jumuiya katika utekelezaji wa maazimio na mipango mbalimbali.

Kwa kifupi, wanasimamia uandaaji wa sera, uchukuaji wa maamuzi, kwa mfano juu ya muelekeo wa shirika na ushirikiano wake na wadau mbalimbali.

Kwa mfano, viongozi hao walijihusisha na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa mwaka 2010-2014. Na baada ya viongozi hao kukamilisha mpango huo, wakaupitisha.

Hivyo hivyo, jumuiya za dini na viongozi wake wanapaswa kusimamia dira zao.

Kwa kifupi, mashirika ya dini hayapaswi kabisa kuwa watazamaji wa matukio ya kila siku katika utendaji wa IRCPT.

Kuna haja ya kuweka mfumo wa utendaji unaohusisha mahusiano ya karibu kati ya mashirika ya dini na jukwaa lao la IRCPT.

Kadhalika, jukwaa hilo linapaswa kuhakikisha kuwa hili linatendeka.

Picha ya hapo juu inaonesha jinsi mashirika ya dini yanavyopaswa kufanya kazi katika kuhakikisha kuwa kuna mrejesho katika utendaji mzima wa IRCPT.

Hata hivyo, kutekeleza haya si kitu rahisi. Kwani mashirika mengi ya dini hujikuta katika hali ngumu kama mwandishi mmoja maarufu, R.S. Trapp ambavyo amewahi kuandika;

"Ni vigumu kuangalia picha ukiwa mwenyewe uko ndani ya fremu ya picha hiyo." Lakini ili uweze kuona vizuri yale unayotaka kuyaona yakitendeka katika jamii yako, unapaswa utoka nje ya fremu ya picha yako.

Maana ya msemo huu ni kwamba unapaswa kuvunja kuta za migawanyiko, kutoaminiana na vitu vyote ambavyo vinatufanya kuwanyanyasa wenzetu.

## 3. Uzoefu wa Kenya

Katika kuwasimulia yaliyotokea nchini Kenya, baada ya uchaguzi mkuu, lakini pia nafasi ya jumuiya za dini ni mojawapo ya majukumu yangu katika mada yangu leo.

Tarehe 31, mwezi Mei, mwaka 2009, niliombwa kutoa mada nchini Zimbabwe juu ya Mchango wa Viongozi wa Dini katika Machafuko yaliyotokea nchini Kenya baada ya Uchaguzi Mkuu, Ujenzi wa Amani, Maridhiano, Kuwatafutia Makazi Wahanga wa Machafuko na Ujenzi Mpya wa Maeneo yaliyoharibiwa wakati wa mapigano.

Mada yangu ilipaswa pia kuonesha michango mibaya ya viongozi wa dini kabla na wakati wa machafuko hayo.

Katika mada yangu, pia nilisema kuwa haikuwa lazima kwa viongozi wa dini kila mara kutofungamana na upande wowote.

Kwamba, walipaswa kupendekeza njia mbadala ambayo ingetoa nafasi kwa watu kuzungumzia namna ya kutatua matatizo yao ya taifa.

Pia niliwataka kutoa nafasi kwa wananchi kuzungumzia matatizo yao kwa uwazi zaidi, wawaruhusu kuuliza maswali magumu na majibu ya maswali hayo wapatiwe.

Ili hili liweze kufanikiwa, kulikuwa na haja ya kutayarisha uwanja wa majadiliano unaokubalika na pande zote katika mgogoro na kwamba, mazungumzo hayo yanapaswa kusimamiwa na viongozi wa dini wanaokubalika na pande husika.

Kwa bahati mbaya, na kwa kweli ni jambo la kusikitisha nchini Kenya pamoja na kuwepo na mifumo mingi na mizuri ya jukwaa la dini, jumuiya za dini nchini humo zilishindwa kukubaliana juu ya haja ya kusimamia ukweli.

Mwaka 2005, jukwaa lililokuwa likijulikana kama Ufungamano, lilivunjika baada ya kutofautiana katika masuala ya dini na katiba.

Jumuiya moja ya dini ilijitoa katika mchakato huo kwa madai kuwa walikuwa wamesalitiwa.

Na kwa kweli, hapa ndipo mvua ilipoanza kutunyeshea jumuiya za dini na wananchi wa Kenya kwa jumla.

Kuanzia hapo, matatizo yakaanza ndani ya dini na jumuiya za kidini.

Na mivutano hiyo hatimaye ikazaa shutuma kati ya dini moja na dini nyingine, hali iliyopelekea kuibuka kwa wasiwasi na kutoaminiana.

Sula la dini na mgogoro wa katiba ukajitokeza tena wakati wa zoezi la mwisho.

Kutokana na kuzuka kwa kutoaminiani, wale waliotaka kuwekwa kwa Mahakama ya Kadhi katika Katiba wakasema bila kutekelezwa hilo walikuwa tayari kufa.

Na wapinzani wa kuwekwa Mahakama ya Kadhi katika katiba wakasema hilo litawezekana tu juu ya maiti zao.

Ni dhahiri kuwa matamko ya pande hizo mbili hayakuwa mazuri, kwani ni ukweli usiopingika kuwa matamko hayo yaliwakilisha misimamo mikali ya pande hizo mbili, misimamo ambayo haikupaswa kutawala maisha ya wananchi nchini Kenya.

Kutokana na kutokuwapo kwa uongozi ambao ungeweza kusimamia mazungumzo kati ya pande hizo mbili zilizokuwa zikihasimiana, baada ya viongozi wa dini kupoteza nafasi yao muhimu katika taifa, hali hiyo iliendelea mpaka wakati wa upigaji wa kura ya maoni juu ya katiba ya Kenya.

Ijapokuwa kura ya maoni hatimaye ilipigwa na Kenya sasa ina katiba mpya, lakini jukwaa la dini likaanguka moja kwa moja.

Mchakato wa Uchaguzi Mkuu nchini Kenya kila mara umekuwa ukikabiliwa na makundi mawili:

- Kundi la kwanza hupiga kura katika namna ambayo serikali mpya pengine ingelisaidia kundi hilo katika kurekebisha uonevu wa zamani uliyofanywa na serikali iliyopita.

- Kundi la pili hupiga kura kwa namna ya kuhakikisha kuwa mfumo na viongozi wa serikali ya zamani unaendelea ili kulizuia kundi lingine lisijelikapata nafasi ya kulipiza kisasi.

Kuzaliwa kwa makundi haya mawili nchini Kenya, kumetokana na matokeo ya historia ya kikabila, kisiasa na kiuchumi.

Kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa kijamii, kiutamaduni na kidini nchini ambako kumechangiwa, kwa kiasi kikubwa na vyombo vya habari visivyowajibika, kumesaidia sana kuleta tatizo hili ambalo Kenya sasa inakabiliwa nalo.

Kwa mfano, vyombo vya habari nchini Kenya vimekuwa na tabia ya kuandika habari za uongo kwamba mgombea fulani anaongoza na kwamba hakuna namna yoyote wafuasi wake watakubali chochote zaidi ya ushindi katika mchakato huo.

Isitoshe, dini na mashirika ya dini pamoja na redio za FM zimeshindwa kutoa suluhisho la aina yoyote ile, katika migogoro hii.

Nao viongozi wa dini baadaye wakajiunga na vikundi vyao vya kikabila huku wakidai kuwa watu fulani walikuwa wanawapiga vita.

Vitendo hivyo vikawafanya viongozi hao wa dini kupoteza sifa ya dhamira ya jamii.

Na kwa bahati mbaya, wakajikuta ndani ya fremu ya picha, hivyo wakapoteza nafasi ya kuona mbele na hivyo kushindwa kuongoza jumuiya zao za dini katika kutafuta suluhisho la kudumu katika migogoro mbalimbali inayozikabili jumuiya zao na taifa kwa ujumla.

Kwa hiyo, viongozi wa dini na mashirika yao siku zote wanapaswa kutojihusisha na siasa zinazowafumba macho na hivyo kushindwa, hatimaye, kushughulikia masuala ya kitaifa.

Viongozi hawa wanapaswa kufuata ukweli na hata wakati mwingine kuwa tayari kabisa kutofautiana, kwa mfano na kiongozi wa siasa ambaye ni mfuasi wa dini yake.

Hali kama hii kwa mfano inaweza kutokea kabisa wakati wa uchaguzi mkuu kama huu unaotazamiwa kufanyika hapa nchini Tanzania.

Siku zote nimekuwa nikisema kuwa viongozi wa dini, kupitia majukwaa yao ya pamoja, wanapaswa kuwa injini au wawezeshaji wa uundwaji wa mfumo unaowajibika wa uongozi wa kisiasa ambao utaruhusu hata kama walio wengi wanapata wanachokitaka, lakini haki na heshima za wachache zinalindwa na sheria ya nchi.

## 4. **Mchango wa mashirika ya dini katika mchakato wa uchaguzi**

Baada ya kufanya uchambuzi mfupi juu ya misingi ya utendaji wa mashirika ya dini, na baada ya kuona michango ya mashirika hayo na viongozi wao katika mchafuko baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya, swali linalopaswa sasa kuulizwa ni je, nini mchango wa mashirika ya dini katika mchakato wa uchaguzi pamoja na kuhakikisha kuwa uchaguzi huo unakuwa huru na wa haki?

Kazi ya kwanza ya mashirika ya dini ni kutafuta na kushughulikia matatizo ya kitaifa bila viongozi wa mashirika hayo kuingiza maslahi yao binafsi. Kwa kifupi, kazi ya viongozi wa dini ni usuluhishi, uwezeshaji na uenezaji wa ukweli.

- Mashirika ya dini, kupitia umoja wa majukwaa yao, yanaweza kusimamia mazungumzo kati ya pande zinazohasimiana. Mashirika hayo yanaweza kufanikiwa katika hili kwa kutofungamana na upande wowote, kwa viongozi wao kujiweka nje ya fremu ya picha zao na kwa kutokuweka mbele maslahi yao binafsi, kisiasa, kitaasisi na kadhalika. Uwezeshaji huo lazima ujengwe kimfumo. Lakini hilo halitoshi. Lazima mfumo huo ukubalike kwa wahusika.

- Kama viongozi wa dini, lazima tujihusishe katika kutoa mwelekeo wa baadaye wa nchi yetu kwa kutoa ushauri, na wakati huo huo tukitangaza utamaduni wa kukubali na kuheshimu. Hili linaweza kudumishwa kwa njia ya ibada kwa kusisitiza dhana nzima ya ukweli na upendo. Pia kwa kuhusisha uraia mwema na maendeleo ya ujamii na mafundisho ya dini.

- Haja ya kutumia misingi ya kidini katika siasa. Tatizo la ilani nyingi za vyama vya siasa inabadilika kila wakati bila wananchi kuona matunda ya ilani hizo. Lakini misingi ya dini haibadiliki. Kama kitu kilikuwa kibaya

kwa binadamu maelfu ya miaka yaliopita, bado kitu hicho kitakuwa kibaya leo.

- Kwa hiyo ni muhimu kwa mashirika ya dini kusimamia, kitaifa, utatuzi wa migogoro ya kisiasa kwa mazungumzo na sio kwa kutumia mfumo wa midahalo. Njia ya mazungumzo husaidia kuleta maelewano wakati midahalo huchochea hisia za watu na kuibua ushindani na hivyo hali hiyo baadaye hupelekea kujenga chuki. Ni muhimu kwa vyama vya dini kujenga utamaduni wa kutatua matatizo kwa njia ya ushirikiano.

- Usimamizi unaohakikisha ujenzi wa nchi kwa ajili ya manufaa ya jamii nzima.

- Kujihusisha kwa vyama vya dini katika mchakato wa uchaguzi mkuu kunapaswa kuanza kutoka ngazi ya chini kabisa. Kuna haja ya kuwahusisha wataalamu wa masuala mbalimbali ili kuahakikisha kuwa hatimaye wanasiasa wanakuja na utekelezaji wa masuala ya maendeleo ambayo yanasimamiwa na maadili ya taifa ambayo yatasaidia katika kujenga umoja, amani na ushirikiano nchini baada ya uchaguzi mkuu.

- Kwa kuwa lengo la vyama vya dini ni kuahakikisha muendelezo wa amani nchini. Mifarakano kati na baina ya wagombea inapaswa kushughulikiwa kabla ya uchaguzi, na sio baada ya uchuguzi. Ni kwa njia hiyo tu chaguzi zitakuwa na matokeo ya kuleta ushindi kwa wote na hivyo kuondoa misuguano isiyo ya lazima.

- Mashirika ya dini yanapaswa kutoruhusu nafasi yao ya usimamizi wa maridhiano na amani mikononi mwa wanasiasa. Hii ni kwa sababu wanasiasa siku zote wana malengo binafsi ya kisiasa ambayo huwa na malengo ya kujitafutia sifa na umaarufu.

- Viongozi wa mashirika ya dini wanapozungumzia masuala kama vile haja ya kuwa na uchaguzi huru na wa haki, wanapaswa kuzungumza kwa umoja na kwa kutumia kikao kimoja. Tukio hilo linapaswa kushuhudiwa na viongozi wote wa juu wa dini mbalimbali katika shirika hilo. Faida ya hili ni kwamba wananchi huwa na imani ya viongozi wao wanapozungumza wakiwa sio tu pamoja, bali pia wakitumia sauti moja. Hapa ndipo viongozi wa dini nchini Kenya walipofanya vibaya. Hawakuonesha umoja, sio tu kwa waumini wao, bali pia kwa wananchi wote wa Kenya kwa ujumla. Kwa kawaida, wananchi hupoteza imani yao kwa viongozi wao mara wanapogundua kuwepo kwa kutoelewana kati ya viongozi hao.

## 5. Mwisho. Wito kuchukua hatua

Kaka na dada zangu. Kama vile baba wa taifa hili, Mwalimu Julius Nyerere, alivyosema wakati wa uhai wake, "inawezekana, timiza wajibu wako'.

Uchaguzi huru na wa haki unawezekana kabisa nchini Tanzania. Timiza tu wajibu wako. Kama viongozi wa dini hapa nchini, mnaheshimiwa sana na waumini wenu. Isitoshe, kama viongozi wa dini mna uwezo mkubwa wa uhamasishaji. Taasisi za imani za kidini zinapatikana kila mahali hata kwenye ofisi za serikali ambazo zimeshindwa kutimiza wajibu wao kwa wananchi.

Kwa hiyo, tutumie nafasi hii katika kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu sio tu unakuwa huru na wa haki, bali pia tunasimamia katika kujenga dhana ya uraia mwema na uongozi adilifu nchini kote, kutoka kwenye mashina mpaka juu katika ngazi ya taifa, kupitia dhana ya uhamasishaji na uwezeshaji.

Lakini si rahisi kufikia malengo haya. Ili tufanikiwe, tunapaswa kujenga umoja kati na baina yetu, kimawazo, kifikra na kivitendo kwa lengo la kujenga msukumo mmoja wa ufanikishaji wa malengo yetu.

Kwa hiyo, tuvunje kuta ambazo zimekuwa zikitutenganisha, tubomoe tofauti zetu amazo zimekuwa zikitufanya tushindwe kukaa pamoja na tuangalie, kwa kina, matatizo na mifumo ambayo kila siku imekuwa ikitufanya tushindwe kupambana na changamoto zinazotukabili kama taifa.

Wakati huo huo, tutakapotoka nje ya fremu ya picha yetu ili tuweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za uchaguzi, tusisahau kushughulikia matatizo ya ndani.

Lazima tukumbuke kuwa kusahau matatizo ya ndani ni sawasawa na mabaharia ndani ya chombo kinachovuja ambacho nje kimezungukwa na maharamia.

Kama wale mabaharia, tunapaswa kuziba kwanza chombo chetu wakati tukijitayarisha kupambana na maharamia waliokizunguka chombo chetu.

Kwa kifupi, tunapaswa kushughulikia matatizo ya ndani sawasawa na matatizo ya nje. Uzoefu unaonesha kuwa mara nyingi tunashughulikia matatizo ya nje na kuacha matatizo ya ndani.

Mkutano huo unatupa nafasi nzuri ya kufanya mazungumzo ya pamoja, ya kina na wazi juu ya matatizo ambayo yamekuwa yakitukabili ndani na kati ya dini zetu, matatizo yanayohusu jamii za taifa letu.

Tunapaswa pia kutumia mkutano huu kupanga mkakati wa namna ya kutatua matatizo yetu, hatua kwa hatua.

Kwa kifupi, tunapaswa kuandaa mpango kazi wa utatuzi wa matatizo yetu. Sisi katika ACRL-RfP, tuko tayari kufanya kazi na nyinyi katika kutatua matatizo yanayolikabili taifa lenu na bara la Afrika kwa ujumla.

Ni matumaini yangu kuwa mkutano huu utawasaidia kujifunza yaliyotokea siku zilizopita, kama vile mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yaliyotokea nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu, na hivyo kushughulikia matatizo yanayowakabili sasa.

Ni matumaini yangu kuwa hili litawasaidia katika kujitayarisha na utatuzi wa matatizo ya siku za usoni.

Kadhalika, ni matumaini yangu kuwa baada ya mkutano huu, mtaandaa mpango rahisi wa utekelezaji ambao sio tu utahakikisha kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2010 unakuwa huru na wa haki, bali pia mtatayarisha mazingira ya utatuzi wa matatizo mbalimbali kwa amani.

Lakini pia, ni matumaini yangu kuwa mtatayarisha msingi wa mchakato wa chaguzi huru na za haki zijazo. Kwa hili, tunapaswa kwanza kabisa tuanze kwa kujiangalia wenyewe.

Asante sana na nawatakia mkutano mzuri.

**Kiambatishi 2: MADA ZILIZOWASILISHWA**

## MCHANGO WA MASHIRIKA YA DINI KATIKA KUHAMASISHA UCHAGUZI HURU NA HAKI (KWA MTAZAMO WA KIELIMU)

**Imetolewa na Ndugu Ebenezer Stafford Mshana, wa Shule ya Sheria, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.**

**Makala iliyowasilishwa kwenye mjadala kati ya KAS na IRCPT kuhusu mchango wa mashirika ya dini katika kuhamasisha uchaguzi huru na wa haki uliofanyika tarehe 11-13 Oktoba 2010, katika Hoteli ya Land Mark jijini Dar es Salaam.**

"….demokrasia ya kweli ina maana zaidi ya kushikilia tu dhana ya uchaguzi huru na wa haki kwa kuwahusisha watu wazima wenye sifa ya kupiga kura, katika muda maalum uliopangwa. Msingi wa demokrasia ni lazima ujengwe katika haki kwa wote katika jamii. Demokrasia inahitaji usawa wa heshima kwa haki za binadamu." (Carlo Fonseka, demokrasia ya kweli ina maana zaidi ya kushikilia uchaguzi huru na wa haki katika muda unaofaa).

### 1. Utangulizi.

Jamii ya Tanzania ni jamii ya kidini, na leo hii zaidi ya theluthi mbili ya watu wake wanajitambua kwamba ni wanajumuiya au kundi la dini moja au nyingine. Ifahamike kwamba taasisi za kidini zinamchango mkubwa sana kwa maisha ya mamilioni ya watanzania katika nyanja za kiimani na hata katika utoaji wa huduma za kijamii kama vile afya na elimu. (Mukandala, R. et al, 2006.1)

Pamoja na hayo, dini isipotumiwa vizuri inaweza kuleta mgawanyiko na kusababisha mgawanyo wa watu katika siasa ambao unaweza kusababisha ugumu katika juhudi za kujenga umoja wa kitaifa. (Mallya, E.T, 2006). Hata hivyo, dini ikitumiwa ipasavyo, inaweza kujenga umoja na mshikamano thabiti wa kitaifa.

Katika kifungu namba 19 ibara ya 2 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeelezwa wazi uhuru wa kuabudu na kuzuia taifa lisijihusishe lenyewe katika masuala ya kidini/ kiibada au katika kuendesha taasisi za kidini. Kifungu hiki kinasema hivi,

"Bila ya kuathiri sheria zinazohusika za Jamhuri ya Muungano, kazi za kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiari ya mtu

binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mambo ya Mamlaka ya Nchi.

Pamoja na hayo, zoezi la uhuru huu wa kuabudu umeegemezwa katika sheria nyingine na katika zoezi linalofanana na hili kwa watu wengine. Kwa hiyo, mtu hawezi kuendesha mambo ya dini yake katika njia ambazo zinakwaza au zinavunja haki za kuabudu kwa watu wengine au umma kwa ujumla. Kwa ufupi, katiba inataka uvumilivu wa dini.

Tanzania ilianzisha tena mfumo wa vyama vingi mwezi Julai, mwaka 1992, kupitia marekebisho ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katiba inaruhusu uhuru wa kuanzisha chama ikizingatiwa kwamba, chama hakiwezi kusajiliwa hadi pale kinapoainisha wazi kwamba "uanachama ni hiari ya mtu, wazi kwa raia wote wa Jamhuri ya Muungano bila kuwa na ubaguzi wa aina yoyote kijinsia, kidini, ubaguzi wa rangi, ukabila, utaalamu au kazi fulani."

Zaidi sana, katiba inaeleza kwamba, hakuna chama chochote cha siasa ambacho kitasajiliwa ikiwa kitakuwa kimetimiza mahitaji kwa ajili ya kupata usajili kama katiba au sera zake "zinakuwa na lengo la kuendeleza au kutangaza matakwa ya imani yoyote au kundi lolote, kabila lolote, kundi la kikabila au ubaguzi wa rangi. Au kwamba kinalenga watu wa sehemu fulani ya Jamhuri ya Muungano."

Hivyo basi, hakuna mwanya wowote wa kuanzisha chama, pamoja na mambo mengine, chenye misingi ya kiimani.

Kwa kuongeza, maadili ya vyama vya siasa, serikali pamoja na tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa msisitizo, imeeleza kwamba vyama vya siasa havitakiwi kutumia vigezo vya dini katika kuhamasisha matukio ya kisiasa, na kwamba havitakiwi kuhamasisha ukabila, udini, ubaguzi wa rangi au jinsia katika kampeni zao za kisiasa. Vivyo hivyo, viongozi wa dini hawaruhusiwi kutumia vyeo na nafasi walizonazo katika kupiga kampeni kwa chama chochote cha siasa au kwa wagombea wakati wa ibada.

## 2. Chaguzi Huru na za Haki.

Chaguzi ni misingi ya hatua za awali za utawala bora. Utawala bora unatetea zaidi kanuni za demokrasia, ambazo ni nguvu za umma zinazotahamali/zinazohisia kwamba serikali inaweza kuwa halali pale tu kwa matakwa ya wale inaowaongoza.

**Matakwa haya yanaweza kulindwa kupitia chaguzi za ushindani wa wengi mara kwa mara.**

Ushindani katika siasa unataka sheria za uchaguzi na njia ambazo zinawapatia wapiga kura njia nzuri ya kubadili serikali pale inaposhindwa kufikia maendeleo na matarajio yao. (Chaligha, 2000.519)

Makubaliano ya kimataifa ya miaka ya hivi karibuni kuhusiana na misingi ya chaguzi za kidemokrasia, na chaguzi ambazo zimeweza kutimiza viwango hivyo kwa kawaida hujulikana kama "huru na haki."

Sheria ya kimataifa imeweka majukumu ya lazima kwa mataifa na mamlaka za uchaguzi kuhusiana na maadili ya uchaguzi.

Katika tamko la dunia la haki za binadamu la mwaka 1948, mkataba wa kimataifa wa mwaka 1966 kuhusu haki za uraia na siasa pamoja na vyombo vingine vya kimataifa, vimeunda masharti makuu mawili kwa chaguzi za kidemokrasia.

(1) Haki sawa ya kupiga kura na sanduku la siri la kupigia kura.

(2) Makubaliano ya kimataifa yanapiga marufuku ubaguzi wa aina yoyote unaojengwa katika misingi ya ubaguzi wa rangi au jinsia.

(3) Unasisitiza haki ya kushiriki katika chaguzi kwa misingi ya "haki sawa ya kupiga kura."

(4) Ili uchaguzi huo upate alama ya "huru na haki", lazima uchaguzi huo utimize na kufikia viwango vya mambo mengine muhimu.

(5) Shughuli za "UCHAGUZI HURU" ni zile ambazo haki za msingi za binadamu na uhuru vinaheshimiwa, hii ni pamoja na.

- Uhuru wa kuongea na kujieleza kwa wapiga kura, vyama vya siasa, wagombea na vyombo vya habari.
- Uhuru wa kujihusisha, ambao ni uhuru wa kuunda asasi kama vile vyama vya siasa pamoja na asasi za kiraia.
- Uhuru wa kukutana (kufanya mikutano), kufanya mishikamano ya kisiasa na kufanya kampeni.
- Uhuru wa kuwafikia na kufikiwa na wapiga kura, kutuma na kupokea habari na ujumbe wa kisiasa na uchaguzi.
- Uhuru wa kujiandikisha kama mpiga kura, chama au mgombea.

- Uhuru wa kuepukana na vurugu, vitisho na shuruti.
- Uhuru wa kufikia vituo vya uchaguzi kwa wapiga kura, wawakilishi wa vyama pamoja na waangalizi walioteuliwa.
- Uhuru wa kuendesha zoezi la haki ya uraia ya kupiga kura kwa siri,
- Uhuru wa kuuliza, kutoa changamoto na kuandikisha malalamiko au vipingamizi bila ya kuwepo kwa matokeo au athari hasi.

Lengo la "UCHAGUZI HURU NA WA HAKI" huwa limefikiwa ikiwa shughuli hizo zimeruhusu uwepo wa uwanja wa tambarare wa kuchezea wa kisiasa, uwanja unaoweza kufikiwa na wapiga kura wote, vyama na wagombea wao. Hii ni pamoja na kuwa na yafuatayo:

- Kuwa na chombo cha Uongozi kinacho jitegemea, adilifu na kisicho fungamana na upande wowote ambao kitasimamia zoezi zima la uchaguzi.
- Haki iliyodhaminiwa na kulindwa na katiba na sheria pamoja na kanuni za uchaguzi.
- Vyama vya siasa pamoja na watu binafsi ni lazima kuwa na nafasi maalumu ya kusimamia/kutetea uchaguzi.
- Uwakilishi sawa wa wapiga kura unaopatikana kupitia sheria za uchaguzi, haki ya kupiga kura iliyoainishwa wazi pamoja na kura za siri.
- Usawa na ulinganifu wa kupata na kuwasilisha taarifa kwa vyombo vya habari.
- Usawa wa nafasi ya kupata elimu ya siasa na elimu ya mpiga kura kwa pamoja na taarifa kwa wapiga kura.
- Uwezo wa kufikia vituo vya kupiga kura.
- Usawa katika kuhudumiwa kwa wapiga kura, wagombea pamoja na vyama vya siasa kwa maafisa wa uchaguzi, serikali, polisi, jeshi pamoja na mahakama.
- Kuwa na uwazi katika zoezi zima la kuhesabu kura.
- Zoezi zima la kupiga kura lisiingiliwe na vurugu,vitisho na shuruti.
- Kusiwe na matumizi mabaya ya rasilimali za umma kwa ajili ya kampeni,

- Ni lazima kuwepo na ushawishi na haki ya utatuzi wa machafuko na manunguniko yanayoambatana na uchaguzi, kabla na baada ya siku ya uchaguzi.

Kutokana na kuongezeka kwa matakwa ya jumuiya za kimataifa tangu mwaka 1990, kumekuwa na asasi mbalimbali za kimataifa ambazo zimeweza kueleza kwa ubora zaidi dhana nzima ya chaguzi "huru na haki " au kuweza kufafanua viwango vya viambatanisho vya chaguzi hizi.

Katika mwaka 1994, umoja wa bunge la kimataifa uliamua kukukubali rasmi tamko la vigezo vya uchaguzi huru na wa haki, ambapo lilitamka haki nyingi za raia, wagombea, vyama na mataifa kama vitu muhimu katika chaguzi huru na za haki. Makubaliano yalisema kwamba, taifa ni lazima kutambua na kutoa vitu vifuatavyo:

- Haki ya mtu kupiga kura bila ya kuwepo kwa misingi ya ubaguzi wa aina yoyote.
- Haki ya kila mtu ya kupata hatua madhubuti, adilifu na zisizokuwa na ubaguzi wowote za uandikishaji wa kura.
- Haki ya kila raia mwenye vigezo, kuandikishwa kuwa mpiga kura, na kwamba ni kwa wale tu ambao hawana vigezo vya kuandikishwa kuwa wapiga kura hawataandikishwa, na kwamba vigezo hivi vielezwe wazi na sheria za nchi, ya kwamba vigezo vinaonekana wazi na si kwa sababu ya maamuzi ya kufikirika ya mtu binafsi.

Katika ngazi za jumuiya za kitaifa na zile zilizo ndani ya jumuiya za kitaifa, mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Chaguzi na Utawala Bora, pamoja na Kanuni na miongozo ya Chaguzi ya umoja wa Nchi zilizopo kusini mwa jangwa la Sahara (SADC), nazo pia zimeeleza bayana maadili ya uchaguzi huru na wa haki.

Kwa Tanzania, katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania imebainisha umuhimu wa kuwa na chaguzi huru na za haki, na hata hizi dhamana za kikatiba zimetafsiriwa kwa undani katika sheria ya nchi ya uchaguzi.

Pamoja na hayo, ili kuweza kujua kama uchaguzi ni huru na wa haki, mtu anahitaji kungalia pande zote mbili, sheria na hali halisi inayotokea na sio kuangalia tu vyombo vya kimatifa, jumuiya za kitaifa au vile vilivyopo ndani ya jumuiya za kitaifa au kwa kuegemea katika yale ambayo yanaelezwa ndani ya sheria. Zaidi ya hayo, pamoja na kuibuka kwa makubaliano katika kanuni za kimataifa zinazoongoza uchaguzi halali, makubaliano ya kupanga vigezo maalumu vya kivitendo katika kuamua kama uchaguzi ni huru na wa haki imebaki kuwa utetezi.

Hata hivyo, asasi za kimataifa zimefanikiwa kupanua vigezo vya msingi ambavyo ni pamoja na kuwa na mahitaji kama “usawa”, “uwazi” na “uwajibikaji”.

Kanuni ya usawa inataka, inasisistiza kuwa kura ya raia mmoja ipewe uzito sawa na zile za watu wengine.

Kuwa wazi, ina maana yakuwa uchaguzi lazima uwe na hatua zinazotabirika, kuwa na matokeo yanayowekwa/kutangazwa wazi na kwamba kuwepo na ulinzi dhidi ya rushwa.

Uwajibikaji unawataka wale wote waliochaguliwa wawe wanapatikana ofisini na kutambua wajibu wao kwa wapiga kura wao.

Wengine wameendelea kufafanua kwamba, kuwe na mtiririko na maelezo ya kina kwa vitu vinavyohitajika kwa ajili ya chaguzi huru na za haki.

Kwa bahati mbaya, kanuni hizo zilizoelezwa kwa kina pamoja na mtiririko wa alama hizo za chaguzi zinatokea kwa nadra sana katika ulimwengu halisia.

Ni kwa sababu ya kufafanua dhana na sio misingi midogo ya uchaguzi unaokubalika, hawakutoa ufafanuzi wa kuridhisha wa kinadharia kuhusu viwango vya uangalizi huru na wa haki, wala mwongozo wa kivitendo kwa waangalizi wa chaguzi.

Kanuni mbalimbali pamoja na vigezo havitoi msaada katika kazi ya kutambua kama jaribio limefikiwa au la, halitoi mwongozo wa jinsi ya kukabiliana na vigezo tata au hata kwa hali ambazo zimekuwa zikififikiwa kwa kiwango cha chini mno, au hata ni uzito gani vipewe vigezo mbalimbali.

Hivyo, kutokana na changamoto hizi, baadhi ya asasi za kusimamia uchaguzi zimeamua kuepuka matumizi ya maneno “huru na haki” kwa sababu maneno haya yanajieleza wazi na yanahukumu.

## 3. Jukumu la asasi za kidini/kiimani katika kuhamasisha chaguzi huru na haki.

Asasi za kidini zinaweza kutimiza jukumu kubwa la kuhamasisha chaguzi huru na za haki kupitia uendeshaji wa miradi ya elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura, kuhimiza uadilifu pamoja na maadili pamoja na kusimamia na kuangalia chaguzi.

4. **Utoaji wa elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura.**

Umuhimu wa elimu ya uraia, ambao hauishii kwenye elimu ya mpiga kura tu, ni elimu ambayo ina mchango mkubwa katika kuhakikisha uwepo wa chaguzi huru na za haki. Demokrasia inataka wapiga kura waelewe kwani ni ukweli usiopingika kuwa uwepo wa hali hii hupunguza, kwa kiasi kikubwa, migogoro ya uchaguzi. Hata hivyo, kabla hatua hii haijafikiwa, kuna haja ya wananchi kuendelea kujihusisha na mazungumzo juu ya mstakabali wa mchakato wa uchaguzi. Uchaguzi katika kila hali unahitaji ufahamu, taarifa na uelewa wa nguvu za kisiasa zinazoshindana katika kufanya maamuzi sahahi kuhusu uteuzi wa sera na njia ya kupaza sauti kwa mahitaji yao.

Hili ni muhimu kwa sababu demokrasia ya kweli inamaana zaidi ya chaguzi huru na za haki.

Elimu ya uraia ni mchakato ambapo umma unapewa ufahamu wa haki na wajibu wa kijamii na kisiasa pamoja na kanuni na shughuli za kiutendaji.

Kwa hiyo, elimu ya uraia inatengeneza ufahamu/uelewa wa shughuli za uchaguzi, ikiruhusu vyama vya siasa pamoja na wagombea kuandaa sera zao katika kuwasaidia wapiga kura kufanya uchaguzi sahihi.

Elimu ya uraia inatumika katika kupanua uelewa katika mambo mbalimbali yanayotolewa na wanasiasa pamoja na wagombea wakati wa uchaguzi, lakini zaidi ya hayo, inawezesha wapigakura pamoja na kuwapa watendaji wa jumuiya/jamii vyombo, taarifa, ujuzi wa kuhamasisha na uelewa wa mabadiliko muhimu ya kisiasa katika kuchangia mabadiliko wakati wa uchaguzi.

Watendaji wa kiserikali na wale wasio wa kiserikali wanalo jukumu la kuhakikisha kwamba elimu ya uraia inatolewa kwa raia/wananchi.

Kwa Tanzania, asasi za kiraia ni pamoja na mashirika/asasi za kidini maarufu kama FBOs ambazo hutoa elimu ya uraia kwa sehemu kubwa ya watu katika jamii kupitia ubunifu wa njia mbalimbali.

Elimu ya uraia huwezesha makundi mbalimbali yenye nia, kwa watendaji wa kiserikali na wale wasio wa kiserikali, kujihusisha na elimu ya kutofungamana kisiasa kwa wapiga kura kwa kutumia njia mbalimbali, zikiwa ni semina na majadiliano kwa njia ya tamthiliya, mashairi na michezo ya kuigiza.

Imetambuliwa tangu uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi wa mwaka 1995, mashirika na asasi za kidini ziliendesha miradi ya utoaji wa elimu ya uraia.

Lakini ili miradi hiyo iweze kufanikiwa, inahitaji kupewa ushirikiano, ili iwe endelevu na ya kudumu.

Asasi hizi za kidini hazitakiwi kufanya kazi kwa ubaguzi na hata kuwa na ajenda tofauti katika kuendesha elimu ya uraia. Kwa hiyo asasi zote za kiraia zinapawa kufanya kazi kwa umoja katika kufikia malengo sawa kwa faida ya wote.

Asasi ya dini haitaweza kufanya kazi kwa usahihi katika utoaji wa elimu ya uraia kama itahamasisha waumini wake kumchagua mgombea kwa kuegemea katika itikadi za kidini, kwa kutaka kumpitisha kwa itikadi hizo na si kwa sababu anafaa kuwa kiongozi mzuri.

Mara nyingi kiongozi asiyefaa huathiri jamii nzima na sio tu wale wasiokuwa na imani kama yake ya kidini au wenye itikadi tofauti za kidini.

Zaidi ya hayo, ni muhimu kuendesha mafunzo ya elimu ya uraia kwa wakufunzi kwa sababu wakufunzi wengi mara nyingine huleta mabadiliko chanya au hasi katika kuelezea demokrasia.

Hakuna mtu anayeweza kumfundisha mwingine kama yeye mwenyewe hana uelewa wa kutosha kuhusiana na mada inayohusika.

Asasi au mashirika ya kidini yanatakiwa kutimiza jukumu la kuelimisha na kutoa mwanga kwa waumini wao kuhusu utakatifu wa asili ya haki ya kupiga kura na kujitoa wenyewe katika kutimiza jukumu la wadau wa demokrasia.

**Uangalizi na usimamizi wa uchaguzi**

Njia mojawapo ambayo mashirika ya kidini yanaweza kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki ni kwa kushiriki kwenye usimamizi na uangalizi. Hata hivyo istilahi hizi,'usimamizi' na 'uangalizi' zinafananishwa katika matumizi, ni vyema kujua kuwa hii ni michakato miwili tofauti lakini inayohusiana kwa karibu.

Uangalizi ni ukusanyaji taarifa na kuzitumia kufanya maamuzi sahihi kuhusu kustahili, ukubalifu na uwazi katika mchakato wa uchaguzi.

Hii inaweza kufanywa na waangalizi wa ndani au wa nje ambao hawawezi kuingilia kwa njia yoyote mchakato wa upigaji na uhesabuji kura.

Kazi za waangalizi ni kupunguza wasiwasi na kutoa ushauri usioegemea upande wowote kwa maafisa wa uchaguzi pale inapohitajika.

Hivyo basi, waangalizi wa uchaguzi ni lazima watathmini mambo mengi ya msingi, ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa uchaguzi, sheria na mfumo wa taasisi za uchaguzi, na mandhari na mazingira ya kisiasa ambamo uchaguzi unafanyika.

Usimamizi ni ukusanyaji taarifa, kutahini na tathmini ya mchakato wa uchaguzi. Mara nyingi usimamizi hufanywa na taasisi za ndani ambazo zinaweza kusikilizwa na wasimamizi kuhusu mapungufu katika upigaji na uhesabuji kura.

Usimamizi na uangalizi wa uchaguzi huwa katika mifumo miwili:

(a) Muda mrefu, kuanzia hatua za mchakato wa uchaguzi

(b) Muda mfupi, hujumuisha shughuli za siku ya upigaji kura. Katika uangalizi wa muda mrefu, waangalizi husimamia hatua zote za mchakato wa uchaguzi, ikiwa ni wakati kabla ya uchaguzi, wakati rasmi au usiyo rasmi wa kampeni; upigaji kura na kuhesabu kura siku ya uchaguzi; kipindi cha baada ya uchaguzi, ujumuishaji na upangaji wa kura, kushughulikia malalamiko na uundaji wa serikali mpya. Mara nyingine ukubalifu wa mchakato wa uchaguzi hujulikana kabla ya siku ya uchaguzi, au inaweza kubadilishwa na mwitikio baada ya upigaji kura.

Usimamizi na uangalizi ni nyenzo muhimu za kufanyia tathmini kama mchakato wa uchaguzi umeendeshwa katika nchi husika umekuwa huru na haki, wazi na siyo wa kutilia shaka. Zaidi, usimamizi na uangalizi husaidia nchi.

Asasi au mashirika ya dini yana jukumu la msingi kabisa la kuhamasisha uadilifu na maadili katika jamii.

Kuhusiana na uhamasishaji wa uchaguzi huru na wa haki, asasi za kidini zinatakiwa kuhakikisha kwamba kanuni za uaminifu na mahusiano ya amani ambayo wao huhubiri yanapanuliwa katika nyanja za kisiasa.

Hasa kwa kuadhibu waumini wake ambao wanajihusisha na vitendo vya rushwa na vurugu, wanaweza kuwa na jukumu la kuhamasisha utamaduni wa chaguzi huru na za haki.

Kushikilia chaguzi, kuepukana, kufanikisha au kubadili migogoro inayohusishwa na uchaguzi kupitia uadilifu na ufikishwaji wa taarifa kwa wakati pamoja na kutambua nguvu na udhaifu wa zoezi zima la uchaguzi.

Katika kutimiza wajibu wao kama waangalizi wa uchaguzi, asasi za kidini ni lazima kuhakikisha kwamba zinaweka bayana kanuni na njia ambazo zinatakiwa kufuatwa na ambazo uchaguzi unafikia katika viwango vya kitaifa, jumuiya za kitaifa na kimataifa kuhusu chaguzi huru na haki.

Mashirika ya dini (FBOs) kwa Tanzania yamekuwa moja ya waangalizi wa chaguzi tangu uchaguzi wa kwanza kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1995.

Kama waangalizi wa ndani, inaaminika kwamba hata katika uchaguzi ujao, mashirika haya yatachangia kwa kiwango kikubwa sana katika kuhakikisha uchaguzi unakuwa wa amani na kusaidia katika kupunguza uwezekano wa vitendo vya rushwa katika uchaguzi.

Pia, mashirika haya dini yanatakiwa kufanya kazi kama waangalizi katika kuhakikisha kwamba zoezi zima la uchaguzi linafanyika kwa uhuru na haki bila ya udanganyifu, vitisho,werevu na rushwa.

Hivyo basi, mashirika ya dini yana jukumu la msingi sana katika utawala na kuhamasisha chaguzi huru na za haki, pamoja na mambo mengine, kwa sababu ni wadau wakubwa wa uchaguzi na wala sio watazamaji tu.

Na jukumu hili linaweza kufikiwa endapo tu mashirika haya ya dini yatafanya kazi kwa umoja katika kufanikisha malengo sawa/ hayohayo.

## 4. Hitimisho.

Chaguzi huru na za haki zinasaidia kujenga na kudumisha utamaduni wa demokrasia, hupunguza migogoro, huchangia katika utulivu wa kisiasa pamoja na maendeleo ya amani, huruhusu raia kutambua mambo yaundayo siasa pamoja na mwelekeo wa baadaye wa kisera kwa serikali za mataifa yao na kuongeza uwezekano wa ubadirishanaji wa madaraka kwa amani kati uongozi mmoja na mwingine. Pia zinasaidia kuhakikisha kwamba wagombea watakaoshindwa katika uchaguzi wakubali ukweli wa matokeo ya uchaguzi baada ya kuwepo kwa ushindani wa haki.

Hata hivyo, kama asemavyo Carlos Fonseka "demokrasia ya kweli ina maana zaidi ya kushikilia chaguzi huru na za haki zinazosimamia misingi ya watu wazima wenye sifa na haki ya kupiga kura na kwa kipindi cha muda unaofaa. Misingi ya demokrasia ni lazima iwe katika haki ya kijamii kwa wote. Demokrasia inataka kuwepo kwa heshima haki za binadamu kwa wote na isiyokuwa na mipaka."

Mwisho, asasi za kidini zina jukumu muhimu la kuhamasisha chaguzi huru na za haki kwa kuendesha miradi shirikishi, endelevu na ya uhakika/ ya kuaminika ya utoaji wa elimu ya uraia, kuhamasisha uadilifu na maadili na kusimama kama waangalizi katika zoezi zima la uchaguzi kupitia uangalizi/usimamizi wa uchaguzi na uangalizi wa uchaguzi.

## MAREJEO.


Chaligha, A.E 2000, "Ethics in Multiparty Electins in Tanzania" ndani ya Jarida la Social Philosophy, juzuu ya 31 namba 4. Winter 2000, 519-523.

Godwin-Gill, G.S 2006. Free and Fair Elections (toleo jipya lililofafanuliwa zaidi). Inter Parliamentary Union. Geneva.

Inter-Parliamentary Union. 1994. Declaration on Criteria for Free and Fair Elections. Inter-Parliamentary Unio. Geneva.

Konrad-Adenauer-Stiftung. 2010. Interfaith Dialogue in Tanzania. The Role of Faith Based Organizations in Good Governance. Konrad-Adenauer Stiftung. Dar es Salaam.

Mallya, E.T 2006. "Religion and Elections in Tanzania Mainland", in Mukandala R. et al. Justice, Rights and Worship. Religion and Politics in Tanzania. REDET. Dar es Salaam,pp.395-415.

Mukandala, R. et al.2006. Justice, Rights and Worship. Religion and Politics in Tanzania. Research and Education for Democracy in Tanzania (REDET). Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania(URT) 1985. National Elections Act. Government Printer. Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania(URT). Political Parties Act of 1992. Government Printer. Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (URT). The Constitution of the United Republic of Tanzania. Government Printer. Dar es Salaam.

# ORODHA YA WASHIRIKI

| S/N | JINA KAMILI | TAASISI | ANWANI |
|---|---|---|---|
| 1 | Epharaim Mkenda | TEC | P.O Box 2133, Dar es Salaam |
| 2 | Geogrey Andrew | Tumainin University | P.O Box 5429, Dar es Salaam |
| 3 | John Anjelus | Tumainin University | P.O Box 1105, Dar es Salaam |
| 4 | Ebenezer Mshana | Shule ya Sheria, Chuo kikuu cha Dar es Salaam. | P.O Box 35093, Dar es Salaam |
| 5 | Kazweba Abdalalh | JUWAQUTA TAIFA | P.O Box 21308, Dar es Salaam |
| 6 | Mohamed S. Lidonge | JUWAQUTA TAIFA | P.O Box Dar es Salaam |
| 7 | Fredrick Bomani | CETA | P.O Box Dar es Salaam |
| 8 | Hindu B. Lilla | IRCPT | P.O Box 5324, Dar es Salaam |
| 9 | Riziki S. Mngwali | Tanzania Women Interfaith Network | P.O Box Dar es Salaam |
| 10 | Pazi Mwinyimvua | TAMPRO | P.O Box Dar es Salaam |
| 11 | Hamisi F. Kasongo | BAHAI FAITH | P.O Box Dar es Salaam |
| 12 | George Kanga | IRCPT | P.O Box 5324, Dar es Salaam |
| 13 | Pafari Fideus | CETA | P.O Box Dar es Salaam |
| 14 | Salim A Zagar | TAMPRO | P.O Box Dar es Salaam |
| 15 | Attilio Tagalile | FREELANCE REPORTER | P.O Box Dar es Salaam |
| 16 | Madua Rashi | TAMPRO | P.O Box Dar es Salaam |
| 17 | Abdallah Tego | TAMPRO | P.O Box Dar es Salaam |
| 18 | Steven A Mmbojo | TADIP | P.O Box Dar es Salaam |
| 19 | Bernard Okok | ACRL | P.O Box 3862233 Nairobi Kenya |
| 20 | Hamza Mtunu | BAKWATA | P.O Box Dar es Salaam |
| 21 | Ramadhani Hamisi | BAKWATA | P.O Box Dar es Salaam |
| 22 | Pascalia Seffu | BAHAI-TWIN | P.O Box 585 Dar es Salaam |
| 23 | Bandala Seffu | BAHAI-YOUTH | P.O Box 585 Dar es Salaam |
| 24 | Dr.C.D. N Kassala | CPT/TEC | P.O Box Dar es Salaam |
| 25 | Bertha Macha | IRCPT | P.O Box 5324, Dar es Salaam |
| 26 | Istrael Mwasese | IRCPT | P.O Box 5324, Dar es Salaam |
| 27 | Judith B. Mndolwa | KAS | P.O Box 6992 Dar es Salaam |
| 28 | Imelda Maboya | Pentecoastl Council of Tanzania | P.O Box Dar es Salaam |
| 29 | Sistus Mallya | Pentecoastl Council of Tanzania | P.O Box Dar es Salaam |
| 30 | Mahad Hassan | KAS | P.O Box 6992 Dar es Salaam |
| 31 | Erasto Ndeuka | KAS | P.O Box 6992 Dar es Salaam |
| 32 | Richard Shaba | KAS | P.O Box 6992 Dar es Salaam |
| 33 | Alhaj Ayoob Omari | IRCPT | P.O Box 5324 Dar es Salaam |
| 34 | Ame Abdulrahamani | AHMADIYYA | P.O Box Dar es Salaam |
| 35 | Shamim Daudi | IRCPT | P.O Box 5324 Dar es Salaam |
| 36 | Asia Hussein | IRCPT | P.O Box 5324 Dar es Salaam |

Jamii ya Tanzania ni jamii ya kidini, na leo hii zaidi ya theluthi mbili ya watu wake wanajitambua kwamba ni wanajumuiya au kundi la dini moja au nyingine. Ifahamike kwamba taasisi za kidini zina mchango mkubwa sana kwa maisha ya mamilioni ya watanzania katika nyanja za kiimani na hata katika utoaji wa huduma za kijamii kama vile afya na elimu.

Pamoja na hayo, dini isipotumiwa vizuri inaweza kuleta mgawanyiko na kusababisha mgawanyo wa watu katika siasa ambao unaweza kusababisha ugumu katika juhudi za kujenga umoja wa kitaifa. Hata hivyo, dini ikitumiwa ipasavyo, inaweza kujenga umoja na mshikamano thabiti wa kitaifa.

Asasi au mashirika ya dini yana jukumu la msingi kabisa la kuhamasisha uadilifu na maadili katika jamii. Ndiyo maana mashirika ya dini yanatakiwa kufanya kazi kama waangalizi katika kuhakikisha kwamba zoezi zima la uchaguzi linafanyika kwa uhuru na haki bila ya udanganyifu, vitisho,werevu na rushwa.

Chaguzi huru na za haki zinasaidia kujenga na kudumisha utamaduni wa demokrasia, hupunguza migogoro, huchangia katika utulivu wa kisiasa pamoja na maendeleo ya amani, huruhusu raia kutambua mambo yaundayo siasa pamoja na mwelekeo wa baadaye wa kisera kwa serikali za mataifa yao na kuongeza uwezekano wa ubadirishanaji wa madaraka kwa amani kati ya uongozi mmoja na mwingine. Pia zinasaidia kuhakikisha kwamba wagombea watakaoshindwa katika uchaguzi wanakubali ukweli wa matokeo ya uchaguzi baada ya kuwepo kwa ushindani wa haki.

Hata hivyo, kama asemavyo Carlos Fonseka "demokrasia ya kweli ina maana zaidi ya kushikilia chaguzi huru na za haki zinazosimamia misingi ya watu wazima wenye sifa na haki ya kupiga kura na kwa kipindi cha muda unaofaa. Misingi ya demokrasia ni lazima iwe katika haki ya kijamii kwa wote. Demokrasia inataka kuwepo kwa heshima haki za binadamu kwa wote na isiyokuwa na mipaka."

Konrad Adenauer Stiftung

**Konrad-Adenauer-Stiftung,**
**S.L.P. 6992, Isimani Road, Upanga**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255 22 2153174**
**kas.tanzania@gmail.com**